Leo yetu ndiyo kesho yetu

# Uelekeo

| ISSN 2953-2787 | Toleo Na. 00057 | Bei Tanzania sh 1,000 | Jumatano Machi 27 - April 2, 2024 |



## Baadhi ya mambo muhimu kujua mwezi wa Ramadhani

Uk. 15

# Huwezi kuwatenganisha Samia, Magufuli - Makonda

■ **Awaonya wanafiki na wanasiasa uchwara**



## Rais atoa bilioni 50/- ukarabati barabara

**Na Mwandishi Wetu, Dodoma**

RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan, ametoa Sh. Bilioni 50 ikiwa ni fedha za dharura kwa ajili ya matengenezo ya barabara zitakazosaidia kuboresha na kukarabati maeneo yaliyoathiriwa na mvua. Uk. 2

## Ziara ya UVCCM ina jambo



Uk.2

## Marekani kuipatia Tanzania bil. 980/-



Uk.3

## Hayawi hayawi sasa yamekuwa

■ **Dege lingine jipya latua Dar, Majaliwa alizindua rasmi**



# Samia atoa bilioni 50/-ukarabati barabara zilizoathiriwa na mvua

**Na Mwandishi Wetu, Dodoma**

RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan, ametoa Sh. Bilioni 50 ikiwa ni fedha za dharura kwa ajili ya matengenezo ya barabara zitakazosaidia kuboresha na kukarabati maeneo yaliyoathiriwa na mvua.

Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, alisema hayo kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu wakati wa ikipitisha vifungu vya Bajeti ya Fungu 98 ya Wizara ya Ujenzi kwa mwaka wa fedha 2024/25 hivi karibuni.

Alisema katika mwaka wa fedha 2024/25 wizara yake kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (Tanroads) itajikita kufanya matengenezo makubwa katika maeneo korofi yaliyoathiriwa na mvua pamoja na kuendelea kukamilisha utekelezaji wa miradi ya barabara na madaraja husus an ya kupunguza msongamano katika miji ya Dodoma, Mwanza, Mbeya, Arusha, Dar es Salaam na Morogoro.

"Nimshukuru Mheshimiwa Rais Dk. Samia ametupatia kiasi cha Sh. bilioni 50 ambazo ni fedha za dharura kwa ajili ya matengenezo ya barabara zitakazosaidia kuboresha na kukarabati maeneo yote yalioathiriwa na mvua," alisema.

Alisema katika jiji la Dodoma Wizara imepanga kupunguza msongamano wa magari kwa kukamilisha ujenzi wa barabara ya mzunguko wa nje wa Dodoma (kilomita 112.3 kwa kiwango cha lami ifikapo Disemba, mwaka huu na kuanza upanuzi wa barabara kuanzia eneo la Mtumba hadi Roundabout ya Safina.

Aidha, alisema baada ya usanifu kukamilika katika eneo la Mtanana Wizara imepanga kuboresha eneo hilo ambalo limekuwa likijaa maji kwa kupandisha tuta la barabara lenye urefu wa kilomita sita pamoja na kuweka makalvati makubwa yatakayoruhusu maji kupita kwa wingi bila athari yoyote.

Kadhalika, alisema Rais Dk. Samia tayari ameshatoa kibali cha kuanza utekelezaji wa miradi 29 ambayo ipo katika hatua za manununzi na utekelezaji wake unatarajiwa kuanza mwaka ujao wa fedha 2024/25.

Kuhusu suala la taa, Waziri Bashungwa alisema ameshatoa maelekezo kwa Mtendaji Mkuu wa Tanroads na tayari wameanza mchakato wa ununuzi wa taa kwa pamoja ili kuwa na viwango na ubora unaofanana pamoja na kupunguza gharama kwa taa zitakazofungwa katika miji na vijiji.



Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, Selemani Kakoso, ameilekeza Wizara kuisaidia Wakala wa Majengo (TBA) na Wakala wa Ufundi na Umeme (Temesa) kuhusu ukusanyaji wa madeni yao kwa Wizara na Taasisi wanazozidai ili fedha hizo ziwasaidie kutekeleza na kumaliza miradi waliopanga.

"Hakikisheni Wizara mnajielekeza kutafuta fedha, angalieni namna ya kuwa wabunifu kutafuta vyanzo vya upatikanaji wa fedha ili zisaidie kulipa madeni ya wakandarasi na kuwezesha miradi kuendelea," alisema.

# Jafo aanika mafanikio makubwa Muungano

**Na Mwandishi Wetu, Dodoma**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Dk. Selemani Jafo, amesema Tanzania imeshuhudia mafanikio makubwa kisiasa, kijamii, kiuchumi, kimazingira, ulinzi na usalama kufuatia Muungano wa Tanganyika na Zanzibar uliodumu kwa miaka 60 sasa.

Amesema mafanikio hayo yanakwenda sambamba na elimu, afya, maji, barabara, umeme, chakula cha kutosha pamoja na ustawi wa jamii kwa ujumla.

Aliyasema hayo jijini Dodoma jana wakati akizungumza na waandishi wa habari akitoa taarifa kwa umma kuhusu mafanikio ya miaka 60 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Alisema kudumu kwa Muungano huo kunatokana na utashi wa dhati wa kisiasa waliokuwa nao waasisi wa Muungano ambao uliwezesha vyama vya siasa vya TANU na ASP kuungana na baadaye kuunda Chama Cha Mapinduzi (CCM) Februari 5, 1977.

Akizungumzia huduma za elimu, alisema shule za msingi zimeongezeka kutoka shule 3,270, 1961 hadi 20,562, mwaka huu.

Alisema kati ya hizo, shule za serikali ni 18,012 na za binafsi ni 2,550 za sekondari pia zimeongezeka kutoka shule 41, 1961 hadi 6,511 mwaka huu, kati ya hizo, 4,892 ni za serikali na 1,619 ni za binafsi.

Kwa upande wa huduma za afya, Waziri Jafo alisema zinaendelea kuimarika kutokana na uwekezaji mkubwa uliofanywa na Serikali katika kipindi chote cha Muungano kutokana na uwekezaji huo, vituo vya kutolea huduma za afya ngazi zote vimeongezeka kutoka vituo 1,343, 1960 hadi vituo 9,662, mwaka huu.

"Kati ya vituo hivyo, zahanati ni 8,043, Vituo vya Afya 1,176, Hospitali za Halmashauri 171, Hospitali zenye hadhi ya Wilaya 182, Hospitali za Rufaa za Mikoa 28, Hospitali zenye hadhi ya Mkoa 34, Hospitali za Rufaa za Kanda 5, Hospitali zenye hadhi ya Kanda 11, Hospitali maalumu sita , Hospitali ya Taifa moja na Hospitali Maalumu za Taifa sita.

"Mafanikio mengine ni kuimarika kwa upatikana wa huduma za maji, umeme na mtandao wa barabara. Upatikanaji wa maji vijijini umeongezeka kutoka asilimia 32, 2000 hadi asilimia 77, 2022," alisema.

Alisema serikali zetu mbili zinaendelea kuweka mazingira wezeshi na rafiki kwa wananchi wa pande zote mbili kufanya kazi kwa uhuru na amani.

Alisema hali hii inaiwezesha Taifa kuendelea kujitosheleza kwa chakula na kwamba imeongezeka kutoka asilimia 90, 2000 hadi asilimia 124, 2022.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Dk. Selemani Jafo






Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi Taifa (UVCCM) Mohammed Ally Kawaida

# Ziara ya UVCCM katika halmashauri ina jambo

**Na Mwandishi Wetu, Same**

MWENYEKITI wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi Taifa (UVCCM) Mohammed Ally Kawaida, amesema katika ziara zake kwenye halmashauri atataka kuona takwimu za fedha na kufahamu jinsi ambavyo asilimia 30 za fedha za miradi zilivyowasaidia vijana.

Alitoa kauli hiyo juzi katika mkutano wa hadhara wa kupokea taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi kwa kipindi cha miaka mitatu ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan katika Jimbo la Same Mashariki mkoani Kilimanjaro.

Alisema serikali iliamua kusimamisha mikopo ya mapato ya ndani ya asilimia 10 kwa ajili ya vijana, kinamama na watu wenye ulemavu kutokana na sababu mbalimbali na kuyataka makundi hayo kuwa na subira kipindi hiki ambacho serikali inaangalia njia nzuri ya kukopesha fedha hizo.

Alisema Rais Samia kwa nia yake ya kuwasaidia vijana, watu wenye ulemavu na wanawake, amekuja na jambo lingine ambapo kwa sasa miradi yote itakayokuwa ikitekelezwa katika halmashauri asimilia 70 ya fedha zake zitashushwa katika halmashauri.

Alisema Rais amebadilisha sheria na kanuni za manunuzi zinazozitaka halmasahauri nchini kutenga asilimia 30 na kwenda kwa makundi hayo maalum ambapo watatakiwa kupewa zabuni.

VITA DHIDI YA VVU, UKIMWI:

# Marekani kuipatia Tanzania bil. 980/-

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Marekani imepanga kuipatia Tanzania Sh. Bilioni 980 kwa mwaka 2024/25 ili kusaidia kutekeleza vipaumbele vya Serikali kupitia Wizara ya Afya katika kupambana na VVU na Ukimwi.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, alisema hayo wakati wa kikao cha kupitisha bajeti ya PEPFAR kilichofanyika katika ofisi ndogo za Wizara ya Afya jijini Dar es Salaam juzi.

"Tunaishukuru sana Serikali ya Marekani kwa kuendelea kuipatia Tanzania msaada kwa zaidi ya miaka 20 kwa ajili ya kupambana na Virusi vya Ukimwi (VVU) na Ukimwi, ambapo kwa sasa watatusaidia Sh. bilioni 980 kwa ajili ya kupambana na ugonjwa huo," alisema.

Waziri Ummy alisema Tanzania kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo, inaendelea kuweka mikakati madhubuti ya kuyafikia makundi ambayo bado yana maambukizi mapya kwa kiwango kikubwa kama vile wasichana rika balehe na wanawake vijana (AGYW) pamoja na vijana rika balehe na wanaume vijana (ABYM).

Kikao hicho kilihudhuriwa na Balozi wa Marekani nchini, Michael Battle na Mtendaji Mkuu wa PEPFAR Duniani, Balozi Dk. John Nkengasong ambapo kwa pamoja, walijadiliana namna ya kuendeleza ushirikiano huo baina ya Tanzania na Marekani katika sekta ya afya.

Balozi Battle aliipongeza Tanzania kwa kuendelea kufanya vizuri katika kufikia malengo kwa asilimia 95.



Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu

## Mafuriko yasomba mmoja, nyumba 100 zazingirwa maji

**Na Mwandishi Wetu, Kilombero**

MTU mmoja anasadikiwa kusombwa kutokana na mvua kubwa kunyesha na nyumba zaidi ya 100 kuzingirwa na maji katika Kata ya Viwanja Sitini na Kata ya Mbasa Halmashauri ya Mji wa Ifakara Wilaya ya Kilombero mkoani Morogoro kuzingirwa na maji kutoka Mto Lumemo.

Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Wilaya ya Kilombero, Haji Muduluka, alithibitisha kuwa hadi sasa zaidi ya wananchi 40 wameokolewa na jitihada za kuokoa wengine zinaendelea.

Baadhi ya wananchi walioathirika wameeleza kuwa wamepoteza chakula na makazi yao kutokana na mafuriko hayo.

Aidha, walisema wanaomba kwa dhati jitihada zaidi za uokoaji kufanywa ili kunusuru maisha yao, hasa kwa kuzingatia mvua zinaendelea kunyesha.

# Shirika lamwaga vifaa tiba kuunga mkono uwekezaji wa Rais Samia

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam Albert Chalamila, amepokea msaada wa vifaa tiba vyenye thamani ya Sh. 38,409,560 kutoka shirika la JHPIEGO ambalo ni wadau wa maendeleo wanaoshirikiana na mkoa katika kuboresha huduma za afya ya uzazi, mtoto na vijana balehe.

Akizungumza katika hafla ya kupokea msaada huo jijini Dar es Salaam jana, Chalamila alilishukuru shirika hilo na kusema katika ndani ya kipindi cha miaka mitatu ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, mkoa wake umeshuhudia uwekezaji mkubwa katika sekta ya afya ya msingi.

Alisema zaidi ya Sh. bilioni 52 zimetumika katika miradi zaidi ya 70 ya ujenzi wa miundombinu na Sh. bilioni sita katika ununuzi wa vifaa na vifaa tiba mbalimbali.

Aliwataka wataalam kuvitumia na kuvitunza vizuri na kuvifanyia matengezo ya vifaa hivyo ili vidumu kwa muda mrefu.

Mkuu wa Mkoa Chalamila alivikabidhi vifaa tiba hivyo kwa Mganga Mkuu wa Mkoa ili vitumike kwa wananchi.

**Zaidi ya Sh. bilioni 52 zimetumika katika miradi zaidi ya 70 ya ujenzi wa miundombinu na Sh. bilioni sita katika ununuzi wa vifaa na vifaa tiba mbalimbali.**




RC Albert Chalamila

## Vijiji 14 kunufaika mradi wa uhifadhi

**Na Mwandishi Wetu, Simanjiro**

VIJIJI 14 vya jamii ya wafugaji wa Wilaya za Simanjiro na Kiteto mkoani Manyara, vitanufaika na mradi wa uhifadhi jumuishi wa mazingira na kuboresha maisha ya jamii.

Jamii ya wafugaji wa vijiji hivyo watanufaika na mradi huo wa miaka minne unaoanza mwaka huu na kumalizika mwaka 2027 utasimamiwa na shirika la Ujamaa Community Resource Team (UCRT).

Mratibu wa UCRT, Edward Loure, alisema hayo Mji Mdogo wa Orkesumet kwenye uzinduzi wa mradi huo uliofanywa na Mkuu wa wilaya hiyo, Suleiman Serera.

Loure alisema kwa Wilaya ya Simanjiro, mradi huo unatarajia kulenga vijiji vya Ruvu Remit, Lerumo, Ngage, Loiborsoit B, Gunge, Lemkuna, Lengasiti, Losoito na Naisinyai.

> **Jamii ya wafugaji wa vijiji hivyo watanufaika na mradi huo wa miaka minne unaoanza mwaka huu na kumalizika mwaka 2027 utasimamiwa na shirika la Ujamaa Community Resource Team.**

# Huwezi kuwatenganisha Samia, Magufuli - Makonda

## ● Awaonya wanafiki na wanasiasa uchwara

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Paul Makonda, amewaonya wanasiasa uchwara, viongozi wanafiki na wanaojipendekeza wakifanya jitihada za kuwatofautisha Rais Dk. Samia Suluhu Hassan na aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano Hayati Dk. John Pombe Magufuli.

Alisema hayo katika halfa ya mapokezi ya ndege mpya Boeing 737-9Max iliyowasili kutoka Seattle, Marekani jana.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Albert Chalamila, alimkaribisha Makonda kusalimia katika hafla hiyo na aliposimama kufanya hivyo, alisema, kwa kuwa mkutano huo haukuwa wa kwake na yeye alipewa heshima ya kusalimia, alitumia fursa hiyo kusema neno moja.

"Ningetamani leo (jana) iwe siku ya mwisho ya unafiki wa viongozi na wanasiasa uchwara wanaopambana kuwatenganisha viongozi hawa.

"Mafanikio haya tunayasherehekea wote kwa sababu Chama ni kimoja, serikali ni ya CCM na ninyi wananchi mliipigia kura.

"Kuna kasumba ya ujinga unaoendelea wa kutaka kumtofautisha Rais Dk. Samia na Dk. Magufuli...huwezi kuwatenganisha hawa watu na viongozi wengi wanafiki wanaotaka kujipendekeza kwa Rais Dk. Samia kila wakipaa jukwaa wanataka kumfanya Samia kama siyo sehemu ya Magufuli," alisema.

Alisema yeye kama Msemaji wa CCM, chama ambacho Rais Dk. Samia na Dk. Magufuli walizunguka na Ilani ya CCM nchi nzima, kila anachofanya Dk. Samia ndicho ambacho alikifanya Dk. Magufuli.

"Na watu hawa (Magufuli na Samia) walisimama wakazunguka katika Taifa hili, wakatafuta kura kwa pamoja, hivyo huwezi kuwatenganisha, na Waziri Mkuu wao yule pale Kassim Majaliwa," alisema.

Mapema RC Chalamila alisema Dar es Salama wanayofuraha kubwa kutokana na mambo makubwa ambayo Rais Dk. Samia ameendelea kuufanyia mkoa huo katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wake.

Alisema mapokezi ya ndege hiyo ni ishara ya ushindi wa kishindo wa kiuongozi anaoendelea nao Rais Dk. Samia.

Akinukuu msemo wa Waswahili, 'chakula cha kufichaficha hunenepesha panya na siyo paka', Chalamila alisema Rais Dk. Samia hakutaka kufichaficha mambo, ametumia pesa kwenda kununua ndege ili wananchi wanufaike.

# Hayawi hayawi sasa yamekuwa

**Na Hellen Mwango**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amesema sekta ya uchukuzi ni muhimu kwa maendeleo ya taifa na kwamba Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, imeimarisha sekta hiyo kwa kuagiza ndege saba na tayari sita zimeshawasili nchini.

Kadhalika, amesema serikali inaendelea na ujenzi wa viwanja vya ndege kwa lengo la kuunganisha mikoa yote ya Tanzania ili kukuza kilimo na biashara.

Alitoa kauli hiyo wakati wa mapokezi wa ndege mpya ya pili ya abiria Boeng 737-9Max yaliyofanyika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA) na kufanya idadi ya ndege zilizonunuliwa na Rais Samia kufikia sita.

Alisema uwepo wa ndege hizo, unachochea ukuaji wa uchumi na ongozeko la utalii nchini.

"Rais ameniagiza nimuwakilishe katika mapokezi ya ndege hii kutokana na yeye kuwa na majukumu makubwa ya kitaifa," alisema na kuongeza:

"Kutokana na umuhimu wa sekta ya uchukuzi, Rais Dk. Samia anaendelea kuwekeza na kuimarisha sekta hii ikiwamo kununua ndege tano za abiria na moja ya mizigo na hivi karibuni ndege ya saba itawasili nchini," alisema.

Alisema uwepo wa ndege hizo, unaongeza tija katika kilimo kutokana na wafanyabiashara kuuza mazao yao nje ya nchi na kuongeza fedha za kigeni.

Alisema ndege iliyowasili jana, itachochea ukuaji wa uchumi kwa kuongeza huduma kwenye usafiri wa anga kutokana na uhakika wa uchukuzi na ni msingi wa kulinda uwekezaji.

"Pia uwepo wa ndege hii na nyingine, kunapunguza umaskini, kunaongeza ajira katika kuongoza taifa letu kwa ukuaji wa uchumi. Hatua hii inaendeleza pale ilipoishia Awamu ya Tano," aliongeza.

Alisema serikali inajenga uwanja mkubwa wa ndege jijini Dodoma utakaoimarisha safari za ndani na nje ya nchi na unatarajiwa kukamilika Novemba, mwakani.

Mbali na ujenzi huo, alisema serikali inafanya ukarabati wa uwanja namba mbili wa JNIA ambao utakuwa maalum kwa matumizi ya ATCL na itasaidia kuboresha huduma kwa usafiri wa anga ikiwamo kutoa huduma bora ukanda wa Afrika Mashariki.

> **"Pia uwepo wa ndege hii na nyingine, kunapunguza umaskini, kunaongeza ajira katika kuongoza taifa letu kwa ukuaji wa uchumi. Hatua hii inaendeleza pale ilipoishia Awamu ya Tano.**



# Waandishi wawili wafariki dunia ajalini

**Na Mwandishi Wetu, Pwani**

WAANDISHI wa habari wawili wa mkoani Lindi wamefariki dunia katika ajali ya gari waliyokuwa wakisafiria kutoka Dar es Salaam kwenda Lindi kugongana na lori eneo la Nyamwage juzi.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa kipolisi Rufiji, SACP Protas Mutayoba, alithibitisha kutokea kwa ajali hiyo majira ya saa saba usiku wa kuamkia jana.

Alisema katika ajali hiyo watu wawili walifariki dunia ambao aliwataja kuwa ni Josephine Kibiriti na Abdalah Nanda na mtu mmoja aliyefahamika kwa jina la Mziray Abedi mkazi wa Lindi alijeruhiwa.

Alisema Josephine ni mwandishi wa habari kutoka kampuni ya Sahara Media Group na Nanda ni mwandishi wa habari kutoka Channel Ten.

Alisema miili ya marehemu hao imehifadhiwa Kituo cha Afyà Ikwiriri na majeruhi anaendelea kupata matibabu katika kituo hicho.



Marehemu Abdalah Nanda



Marehemu Josephine Kibiriti




# VETA wapanda miti 40,000 wakimuunga mkono Samia

**Na Mwandishi Wetu, Dodoma**

WATUMISHI wa Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) nchini wameungana na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan katika kampeni ya kutunza mazingira kwa kupanda miti zaidi ya 40,000 kuelekea maadhimisho ya miaka 60 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Akizungumza wakati wa zoezi la upandaji miti makao makuu ya VETA, jijini Dodoma jana, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa VETA, CPA Anthony Kasore, alisema tukio la kupanda miti limefanyika kwenye vituo vya taasisi hiyo nchin.

Alisema kazi waliyofanya ni utekelezaji wa maagizo ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwamba kila mwananchi, taasisi na jamii yote kutunza mazingira kwa kupanda miti.

Kasore aliwataka watumishi hao kutunza miti iliyopandwa na kuhakikisha inakua na ikiwamo kuonyesha maana halisi ya kutunza mazingira katika maeneo yao.

"Tunaungana na Rais katika maagizo yake, tupande na kutunza miti hii…nasisitiza tukatunze miti hii ili ikue na kutupa uhai pamoja na kuboresha muonekano wa mazingira yetu," alisema.

Aidha alimshukuru Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) kwa kutoa miti hiyo bure na kuahidi kuendeleza ushirikiano katika shughuli mbalimbali za uhifadhi wa misitu na utunzaji mazingira.

Kwa upande wake Ofisa Misitu wa TFS Kanda ya Kati, Jenipha Elius, alisema anaamini miti hiyo itatunzwa na kukua vizuri kwa kuzingatia kuwa inafuata hatua zote muhimu za kitaalamu za upandaji wake.

"Ninyi kama watumishi mjenge utamaduni wa kupanda miti kwenye maeneo mnayoishi ili mjipatie faida mbalimbali ikiwamo kupata hewa safi pamoja na matunda bado naendelea kuwakaribisha kupata miti bure kutoka TFS," alisema.

Naye mtumishi wa VETA makao makuu, Furaha Paul alisema anaona fahari kupanda miti ambayo itanufaisha watanzania wengi kwa miaka mingi ijayo.

"Kwa kweli najisikia furaha kushiriki kwenye tukio hili la kihistoria kwa kuwa naamini miti hii itatumiwa na sisi, watoto wetu, wajukuu hadi vitukuu vyetu," alisema.

Kilele cha maadhimisho ya miaka 60 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar kinaazimishwa kila mwaka 26 Aprili.

"
Ninyi kama watumishi mjenge utamaduni wa kupanda miti kwenye maeneo mnayoishi ili mjipatie faida mbalimbali ikiwamo kupata hewa safi pamoja na matunda.

# Maoni ya Mhariri & Uchambuzi

## HII NI KERO

## Kupiga na kusikiliza simu kwenye vivuko vya zebra

BAADHI ya watu wamekuwa na tabia ya kutumia simu zimu zao kwa kupiga, kuzungumza, kupokea ama hata kuchat kwa simu zao wakati wakivuka kwenye alama za pundamilia (zebra) bila kujali usalama wao, wa wenzao na vyombo vya moto.

Hii ni kero kwa madereva wa magari na vyombo vingine vya moto kwani eneo hilo linapaswa kutumika na waenda kwa miguu kwa uangalifu ili kuepusha ajali.

Ni busara kuacha matumizi ya namna hiyo hata kama simu itaita ukiwa unavuka eneo hilo, usipokee badala yake subiri mpaka umalize kuvuka na kuwa katika eneo salama.






MAONI YA MHARIRI

# Watendaji ATCL kazi kwenu

JANA, kampuni yetu ya ndege, Air Tanzania Company Limited (ATCL) ilipokea ndege mpya aina ya Boeng B737-9Max, yenye uwezo wa kubeba abiria 181.

Taarifa zilizotolewa jana wakati ndege hiyo inapokelewa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa kwa niaba ya Rais Samia Suluhu Hassan zilionesha kwamba ACTL imefikisha ndege 15 ambapo 14 zimenunuliwa na serikali na nyingine ni ndege ndogo aina ya Dash 8-Q300 ambayo ilikuwepo kabla ya ufufuaji wa kampuni hiyo ulioanza mwaka 2016.

Kwa mujibu wa Waziri Mkuu, hiyo ni ndege ya saba kununuliwa na Serikali ya Rais Samia na tayari ndege sita zimeshawasili nchini.

Lakini cha kufurahisha ni jana kusikia kutoka kwa Mtendaji Mkuu wa ACTL, Mhandisi Ladislaus Matindi kwamba kupitia mpango mkakati wa ATCL wa pili wa miaka mitano ambao ulianza mwaka wa fedha 2022-2023, ATCL inategemea kupokea ndege nyingine mpya ya masafa marefu mwezi Aprili mwaka huu. Alisema lengo ni kufikisha ndege 20.

Tunapongeza hatua iliyofikiwa lakini tunadhani kwamba malengo yawe ni kufikisha ndege hata 100 na kukamata biashara ya ndege katika ukanda wetu huu wa Afrika Mashariki na Kati ambao unasemekana kwamba umeshikiliwa na Ethiopia katika biashara hiyo.

Hi ni kwa sababu ya faida za kuwa na ndege kama alivyosema Waziri Mkuu Kassim Majaliwa ndio maana tunapendekeza hivyo. Baadhi ya faida alizotaja Waziri Mkuu ni kuchochea ukuaji wa uchumi na ongozeko la utalii nchini. Uwepo wa ndege pia unaongeza tija katika kilimo kutokana na wafanyabisahara kuuza mazao yao kwa wingi nje ya nchi, hususani yanayoharibika haraka na kuongeza fedha za kigeni.

Lakini lingine ni ukweli kwamba, mbali na nchi kupata fahari ya kumiliki ndege zetu wenyewe, lakini ndege hizi pia zinaongeza ajira kwa vijana wa Kitanzania.

Tunaamini kwamba menejimenti na wafanyakazi wa TTCL wanaoendesha shirika hili kwa niaba yetu watachapa kazi kwa uadilifu na ubunifu wa hali ya juu ili kuhakikisha kampuni inaongoza, si tu kwa kuwa na ndege nyingi lakini kwa huduma bora barani Afrika. Tukidhamiria inawezekana.

Ni vyema pia serikali yetu ikaendelea kuwa karibu na kuisimamia ATCL ili kuhakikisha inakua haraka na kuleta tija na yeyote atakayeonekana ni mzigo katika kuipeleka mbele ATCL apigwe chini mara moja.


## Wasiliana nasi

**Mhariri Mkuu:** +255713263775 / +255748115000
**Mhariri wa Habari:** +255753333330
**Mhariri Michezo:** +255787559090
**Meneja Masoko/Biashara:** + 255718480406 / + 255733768825
**S. L. P:** 15110, Dar es Salaam
**Makao Makuu Mtaa:** Barabara ya Morogoro
**Jengo la:** Aura Mall
**Chumba Cha Habari:** +255 (0)222151532
**Email:** uelekeohabari@gmail.com


## JICHO LANGU

# Ndege mpya kuimarisha uchumi na utalii nchini

UJIO wa ndege mpya ya Boeing 737-9Max nchini, unafanya ndege zote zilizonunuliwa kufuatia hatua ya Serikali ya Awamu ya Tano na kuendelezwa na Serikali ya Awamu ya Sita kufufua Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) kufikia 14 sasa. Bado Serikali inaendelea kununua ndege nyingine.

Mapokezi ya ndege hiyo yaliyofanyika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA) ikitokea Seattle, Marekani, yalionesha jana jinsi Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, anavyosimamia kwa vitendo Ilani ya Uchaguzi ya CCM.

Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Paul Makonda, anasema wanasherehekea mafanikio hayo kwa sababu Chama ni kimoja, Serikali ni ya CCM na wananchi ndiyo waliipigia kura.

Uamuzi wa Serikali kuifufua ATCL kwa kununua ndege mpya umewafanya Watanzania kutembea kifua mbele, kufuatia unyong'onyevu wa muda mrefu waliokuwa nao kwa shirika lao kukosa ndege za uhakika kwa safari za kibiashara za ndani na za kimataifa.

Kwa muda huo mrefu, baadhi ya mataifa jirani yalitumia kikamilifu ombwe hilo kwa kujinufanisha kiuchumi huku wakizitangaza nchi zao.

**Mathalani, watalii waliokuwa wakija nchini, walilazimika kutumia ndege za mashirika ya nje tofauti na sasa ambapo wanaweza kutumia ndege zetu ambazo nyingi zimebeba majina kama Olduvai Gorge na kadhalika vivutio ambavyo vilivyopatikana katika Hifadhi za Taifa.**

Mathalani, watalii waliokuwa wakija nchini, walilazimika kutumia ndege za mashirika ya nje tofauti na sasa ambapo wanaweza kutumia ndege zetu ambazo nyingi zimebeba majina kama Olduvai Gorge na kadhalika vivutio ambavyo vilivyopatikana katika Hifadhi za Taifa.

Lakini sasa hivi, ujio wa ndege hizo unafanya baadhi ya nchi zilizokuwa zikinufaika na ATCL kukosa ndege za uhakika kuona husda.

Haya ni mafanikio ya kishindo ambayo wenye husda iwe ni nchi au mtu mmoja mmoja kamwe hawawezi kuyafurahia.

Rais Dk. Samia ameendelea kuboresha usafiri wa sekta ya anga ambayo sasa hivi inashika kasi na katika kipindi cha miaka mitatu tu, Watanzania wameshuhudia mafanikio makubwa yanayowafanya watembee kifua mbele.

# Wajue Islamic State waliohusika shambulio la Moscow na kuua 133

**Na Mwandishi Maalum**

LICHA ya majaribio ya Rais Vladimir Putin na vyombo vya habari vinavyodhibitiwa na Serikali ya Urusi kulaumu Ukraine kwa shambulio baya la Ijumaa iliyopita katika ukumbi wa michezo wa Moscow, maelezo zaidi yanaibuka kuhusu kundi la wanajihadi la IS-K ambalo limedai kuwa ndilo lililohusika na shambulio hilo.

### IS-K NI NANI AU NI NINI?

IS-K ni kifupi cha Islamic State-Khorasan. Ni mshirika wa kikanda wa kundi la kigaidi lililopigwa marufuku kimataifa la Islamic State linalolenga Afghanistan, Iran na Pakistan.

Kundi hilo limejipa jina la Khorasan kwa kuwa hilo lilikuwa sehemu ya ukhalifa wa kihistoria wa Kiislamu unaozunguka nchi hizo, na pia kuelekea kaskazini hadi Asia ya Kati.

IS-K limekuwapo kwa miaka tisa sasa, lakini katika miezi ya hivi karibuni, limeibuka kuwa tawi hatari zaidi la kundi la Islamic State, lenye uwezo wa muda mrefu na sifa ya ukatili wa kupindukia.

Pamoja na kile kilichosalia cha uongozi mpana wa kundi hilo nchini Syria na Iraq, IS-K inapania kuwa na ukhalifa wa kitaifa wa Kiislamu unaotawaliwa kupitia tafsiri kali ya Sharia, sheria ya Kiislamu.

Nchini Afghanistan, linaendesha uasi wa hapa na pale, lakini bado ni mbaya dhidi ya watawala wa nchi hiyo, Taliban, ambao inawapinga kwa misingi ya itikadi kali.

### JE, IS-K ILIWAHI KUFANYA MASHAMBULIZI HAPO AWALI?

Ililenga uwanja wa ndege wa Kabul mwaka 2021 kwa bomu la kujitoa mhanga na kuua Waafghanistan 170 na wanajeshi 13 wa Marekani.

Mwaka uliofuata, lililenga Ubalozi wa Urusi mjini Kabul na kuua watu wasiopungua sita na wengine kujeruhiwa.

Kundi hilo limefanya mashambulizi ya kiholela kwenye wadi ya wazazi, vituo vya mabasi na polisi.

Januari, mwaka huu, IS-K ilifanya shambulio la mabomu mara mbili kwenye hekalu huko Kerman, Iran na kuua karibu Wairani 100.

Nchini Urusi, imefanya mashambulizi mengi madogo madogo, ya hivi karibuni zaidi yakiwa mwaka 2020 na tayari mwaka huu, FSB, huduma ya usalama ya ndani ya Urusi, inasema imesimamisha njama kadhaa za ugaidi.



### WASHAMBULIAJI WALIKUWA KINA NANI?

Kulingana na vyombo vya habari vya Serikali ya Urusi, wanaume wanne waliokamatwa na kushtakiwa, wote ni Watajiki kutoka Jamhuri ya Asia ya Kati ya Tajikistan, iliyokuwa sehemu ya Muungano wa Sovieti.

Ni dhahiri kutokana na kufikishwa mahakamani kwa kupigwa na michubuko kwamba wamekuwa wakihojiwa kwa ukali hadi kufikia hatua ya kuteswa.

Tatizo la hilo ni kwa mujibu wa kanuni za kimataifa, maungamo yao hayatakuwa na thamani - watu watasema chochote ili kupunguza maumivu, ikiwa ni pamoja na kukiri kwa simulizi ambayo si ya kweli.

Ripoti zimeibuka kuwa mmoja wa wanaume hao, alionekana akifanya ufuatiliaji wa ukumbi huo mwanzoni mwa mwezi Machi, wakati ambapo Marekani iliionya Urusi kuwa kuna tishio la kutokea kwa shambulio la kigaidi kwenye eneo la umma - onyo ambalo Kremlin ililipuuza wakati huo. "propaganda".

Ripoti nyingine inasema takribani wawili wa washambuliaji waliwasili nchini Urusi hivi karibuni, ikimaanisha kuwa hii ilikuwa "timu ya wapiganaji" iliyotumwa na IS-K, badala ya chumba cha kulala cha wakazi.

### KWANINI WAMEILENGA URUSI?

Kuna sababu kadhaa

IS-K huwachulia nchi nyingi wengi ulimwenguni kuwa maadui wao.

Urusi iko juu katika orodha yao, pamoja na Marekani, Ulaya, Israel, Wayahudi, Wakristo, Waislamu wa Shia, Taliban na watawala wote wa mataifa yenye Waislamu wengi, ambao wanawaona kuwa "waasi".

Uadui wa Islamic State kwa Urusi unakumbukwa nyuma kwenye vita vya Chechnya katika miaka ya 1990 na mapema miaka ya 2000, wakati vikosi vya Moscow vilipoharibu mji mkuu wa Chechnya, Grozny.

Hivi karibuni, Urusi iliingia katika vita vya wenyewe kwa wenyewe vya Syria kwa upande wa mshirika wake, Rais Bashar al-Assad, na Jeshi la Anga la Urusi limefanya milipuko isiyohesabika ya waasi na raia na kuua idadi kubwa ya kundi la Islamic State na Al-Qaeda-wapiganaji wanaohusishwa.

Huko Afghanistan, IS-K inaiona Urusi kama mshirika wa Taliban, ndiyo sababu walishambulia Ubalozi wa Urusi huko Kabul mwaka 2022.



Kisha kuna masuala kadhaa ndani ya Urusi yenyewe.

Urusi inatazamwa na IS-K kama nchi ya Kikristo sana na video yao ilitumwa baada ya shambulio la Moscow inazungumza juu ya kuua Wakristo.

Tajik na wafanyakazi wengine wahamiaji wa Asia ya Kati wakati mwingine wako chini ya kiwango cha unyanyasaji na tuhuma na FSB inapojaribu kumaliza mashambulio ya kigaidi.

Hatimaye, Urusi , taifa ambalo kwa sasa liko kwenye vita vyake vikali na jirani yake Ukraine, huenda ikawa ni shabaha inayofaa ya fursa kwa IS-K, mahali ambapo silaha zilipatikana na askari wa adui kuangushwa.

### TUSICHOKIFAHAMU

Kuna maswali kadhaa ambayo hayajajibiwa kuhusu tukio zima.

Kwa mfano, kwa nini washambuliaji walitangatanga wapendavyo kwa karibu saa moja kuzunguka Ukumbi wa Crocus bila hisia zozote za uharaka?

Katika nchi ambayo polisi na huduma maalum, haswa FSB, wako kila mahali, watu hao wenye silaha walifanya kama wanajua kwamba hawataingiliwa na timu ya polisi ya SWAT.

Kisha kuna silaha, si tu bunduki, lakini zenye nguvu, za kisasa. Je, waliwezaje kuzipata na kuzisafirisha bila kutambuliwa kwenye ukumbi huo?

Ukamataji wao wa haraka pia unashangaza.

Tofauti na wapiganaji wengi wa kijihadi kwenye uvamizi kama huu, wanaume hawa hawakuwa wamevaa fulana au mikanda ya kujitoa mhanga.

Na hata hivyo, haikuchukua muda mrefu kwa mamlaka za Urusi, mamlaka zile zile za Urusi ambazo zilishindwa kuzuia njama mbaya zaidi ya ugaidi katika miaka 20 iliyokuwa ikitokea mbele ya macho yao, kuwakusanya washukiwa na kuwapeleka mahakamani.

Haya yote yanawafanya baadhi ya wachambuzi kutafakari kuhusu aina fulani ya kile kinachoitwa "kazi ya ndani" na Kremlin, au "operesheni ya uwongo ya bendera" ili kupata uungwaji mkono wa watu wengi kwenye vita dhidi ya Ukraine.

Hata hivyo, hakuna ushahidi mgumu wa kuunga mkono nadharia hiyo na ujasusi wa Marekani umethibitisha kwamba kwa maoni yao, ni Islamic State iliyohusika na shambulio hilo baya.





# Kutoka jela hadi kuwa Rais mwenye umri mdogo Afrika

"KAMWE sikuwahi kuzingatia kujiingiza katika siasa," anasema mtoza ushuru huyo wa zamani na mume wa wake wawili.

Wachache walikuwa wamesikia kuhusu mwaka mmoja uliopita na sasa anatazamiwa kuwa Rais.

Kuinuka kwa njia ya ajabu kwa Bassirou Diomaye Faye, kunafikia kipindi cha hali ya juu katika siasa za Senegal ambazo ziliwavutia watu wengi.

Miezi ya kukaa jela pamoja na mshirika na mwanasiasa mwenye ushawishi, Ousmane Sonko, iliisha ghafla, wawili hao wakiachiliwa wiki moja kabla ya uchaguzi wa urais.

Sasa 'Bwana Safi', kama anavyoitwa kwa jina la utani, lazima aanze kufanyia kazi mageuzi makubwa aliyoahidi.

"Anayependa utaratibu" na "asiye wa kujionyesha," ni maneno yanayotumiwa mara nyingi kuelezea mtoza ushuru huyo wa zamani ambaye alisherehekea siku yake ya kuzaliwa ya miaka 44 juzi Jumatatu.

Faye, anakumbuka kwa furaha maisha yake ya kijijini huko Ndiaganiao, ambapo anasema yeye hurudi kila Jumapili kufanya kazi za shamba.

Upendo na heshima yake kwa maisha ya kijijini, inalingana na kutokuwa na imani kubwa na wasomi wa Senegal na walio katika siasa za sasa.

> **Itabidi ashughulikie uhalisia wa bajeti kwa kuanzia... Lakini naona kwamba ana matamanio mengi," Waziri Mkuu wa zamani, Aminata Touré, ambaye alihudumu chini ya Rais anayeondoka Macky Sall, anaiambia BBCkisheria na kukuza jamii inayoshirikishwa zaidi na yenye usawa.**

"Hajawahi kuwa waziri na hakuwa kiongozi wa serikali, hivyo wakosoaji wanahoji ukosefu wake wa uzoefu," mchambuzi Alioune Tine aliambia BBC.

"Lakini, kwa mtazamo wa Faye, watu wa ndani ambao wameendesha nchi tangu mwaka 1960, wameshindwa kwa kiasi kikubwa."

Kupambana na umaskini, ukosefu wa haki na ufisadi ni ajenda kuu ya Faye. Walipokuwa wakifanya kazi katika Hazina ya Kitaifa , yeye na Sonko, waliunda jopokazi la muungano ili kukabiliana na ufisadi.

Makubaliano ya gesi, mafuta, uvuvi na ulinzi, lazima yote yajadiliwe upya ili kuwahudumia vyema watu wa Senegal, anasema Faye.

Anaanzisha enzi ya "uhuru" na "mpasuka" kinyume cha zaidi ya hayo, aliwaambia wapiga kura, na hiyo ni kweli hasa kwa uhusiano na Ufaransa.

Rais mteule wa Senegal, anasema kuwa ataondoa sarafu ya CFA franc ambayo inakosolewa sana, ambayo imeegemezwa kwenye Euro na kuungwa mkono na mkoloni wa zamani Ufaransa.

Faye anataka kubadilisha sarafu mpya ya Senegal, au eneo la Afrika Magharibi, ingawa hii haitakuwa rahisi.

"Itabidi ashughulikie uhalisia wa bajeti kwa kuanzia... Lakini naona kwamba ana matamanio mengi," Waziri Mkuu wa zamani, Aminata Touré, ambaye alihudumu chini ya Rais anayeondoka Macky Sall, anaiambia BBC.

Kuimarisha uhuru wa mahakama na kuunda nafasi za kazi kwa vijana wengi wa Senegal, pia ni vipaumbele muhimu kwa Faye ambayo mtangulizi wake, hakuyatilia umuhimu, Touré anaongeza.

Yeye siyo kigogo pekee wa kisiasa ambaye amemuunga mkono Faye mwenye umri wa miaka 44 - Rais wa zamani Abdoulaye Wade, alifanya vivyo hivyo siku mbili tu kabla ya kura ya juzi Jumapili.

Ni mabadiliko ya ajabu kwa Faye ambaye alikaa gerezani miezi 11 iliyopita kwa mashitaka ya uasi na miaka mingi zaidi kabla ya hapo chini ya kivuli cha mshirika wake.

**'Bassirou ni mimi'**

Bassirou Diomaye Faye, alitangazwa Februari, mwsaka huu kama mgombea anayeitwa "Mpango B", akichukua nafasi ya kigogo wa upinzani, Ousmane Sonko. "Ningesema hata ana uadilifu zaidi kuliko Sonko," alisema kwa majigambo.

Wanaume wote wawili walianzisha chama ambacho sasa kilivunjwa cha Pastef, wote ni watoza ushuru na wanaume wote walijikuta wamefungwa mwaka jana kwa mashitaka ambayo walisema yalichochewa kisiasa.

Sonko aliishia kuhukumiwa kwa makosa mawili, jambo lililomaanisha kwamba alizuiwa kushiriki uchaguzi, hivyo Faye akaingilia kati.

"Bassirou ni mimi," Sonko aliwaambia wafuasi hivi majuzi. "Ni pande mbili za sarafu moja," mwenzake wa Pastef Moustapha Sarré, anakubali.

Hii imesababisha ukosoaji kwamba Faye ni "Rais kwa chaguo-msingi".

Si hivyo, asema mchambuzi Tine. Lakini uhusiano wa wawili hao, unaweza kuleta mtindo mpya wa uongozi.

"Labda wataanzisha mtindo wa kujitenga na mfumo wa urais wa kuwa na mkuu wa nchi mwenye mamlaka yote'

"Sonko bila shaka ni kiongozi asiyepingwa wa Pastef - Kilelezo haswa ..., lakini wawili hao wamekuwa na nguvu ya ushirikiano na kutegemeana."

Awali, Faye hakutaka kujihusisha na siasa. "Haijawahi kuniingia akilini," alisema mwaka 2019 wakati akikumbuka utoto wake.

Mmoja wa mashujaa wa Faye, ni mwanahistoria wa Senegal, marehemu Cheikh Anta Diop - ambaye kazi yake inaonekana kama mtangulizi wa Afrocentrism-dhana ya kuipigania Afrika na itikadi zake. Wote wanaonekana kama wafuasi wa mrengo wa kushoto wa kuunga mkono sera zinazoigemea Afrika iliyoungana.

Matokeo ya mapema yalipokuja siku ya Jumatatu yakionyesha Faye anatazamiwa kupata ushindi, watu katika mji mkuu, Dakar, walisherehekea kwa kupiga honi za gari na kuimba kwa sauti kubwa ya muziki.

Mwitikio kutoka kwa masoko ya kimataifa, haukuvutia kwa kiasi hicho, huku dhamana za dola za Senegal zikishuka hadi kiwango cha chini kabisa katika kipindi cha miezi mitano. Shirika la Habari la Reuters liliripoti kuwa wawekezaji wana wasiwasi kuwa uongozi wa Faye huenda ukapuuza sera za nchi zinazofaa kibiashara.

Awali, uchaguzi ulikuwa ufanyike mwezi uliopita, lakini Sall aliahirisha saa chache kabla ya kampeni kuanza na kusababisha maandamano makubwa ya upinzani na mgogoro wa kidemokrasia.

Wagombea wengi walikuwa na muda mchache mno wa kujiandaa mara tu tarehe mpya ya uchaguzi ilipowekwa, lakini Faye alikuwa na zaidi ya wiki moja tu baada ya kuachiliwa kutoka jela.

Licha ya kipindi kifupi cha kampeni, raia wa Senegal walikuwa wameshikilia kwamba watajitokeza na kutumia kura yao, Christopher Fomunyoh, wa Taasisi ya Kitaifa ya Kidemokrasia ya Mambo ya Kimataifa, aliiambia BBC Newsday.

"Senegal iko katika mchakato wa kuthibitisha kwamba demokrasia inaweza kujisahihisha na kuja kuwa na nguvu na uthabiti zaidi."

Na mtihani wa kweli kwa 'msafishaji' wa Senegal ndiyo umeanza.

*Leo yetu ndiyo kesho yetu*

Uelekeo

JARIDA | Jumatano Machi 27-April 2, 2024 |

# Jungu kuu




Jarida hili haliuzwi



# Dk. Samia anavyowaumbua wapinzani uchwara!

UK. 12 & 13

# Vijana anzisheni familia, msiangamie kwa kukosa maarifa

**Na Dkt. Felician Kilahama**

Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa yote hasa kwa mwaka huu 2024 jinsi anavyoendelea kutulinda na kutujaslia mema ikiwa ni pamoja na kuimarisha afya zetu.

Hata hivyo, Neno la Mungu linatutia moyo tunapoambiwa 'tusiogope' maana Muumba wetu yupo pamoja nasi na hatatuacha: 'mapenzi yake yatimizwe'.

Kadhalika, tunapaswa kuwa wa kiasi na wenye uvumilivu toshelezi huku tukizitumia fursa tulizonazo kwa weledi mkubwa, akili na maarifa wakati huohuo, tukimtukuza Mungu aliye Alfa na Omega.

Tanzania tunayo changamoto kubwa kuhusu hatima za vijana wetu hasa wa kiume kwa maisha yao sasa na baadaye.

Nimethubutu kusema hivyo baada ya kuona majira yanavyokwenda, nyakati zinapita na miaka kuzidi kuongezeka lakini mwelekeo wa vijana wengi umekuwa siyo wenye kuletafaraja kwenye familia zatu.

Huko nyuma niliwahi kuekeza kuwa tangu mwanzo Mungu aliumba mume na mke, akawaweka kwenye Bustani nzuri ya Edeni.

Mwanamume akiwa mzaliwa wa kwanza akapewa madaraka ya kuisimamia na kitunza Bustani pamoja na familia na mwanamke akiwa msaidizi wake wa karibu.

Hata hivyo, katika mazingiara ya sasa, vijana wetu wa kiume (ingawa siyo wote) lakini katika ujumla wao; wamepoteza dira na umuhimu wa kulinda "Urithi" tuliopewa tangu kuumbwa kwa Adam na Hawa (Eva) ambao ndiyo binadamu wa kwanza kuishi kwenye sayari iitwayo Dunia.

Jambo la kushangaza ni kuona vijana walio na umri wa kuoa waishio mijini na vijijini, hawana hamu kabisa ya kuwa na familia (kuoa/kuzaa watoto).

Ukiwadadisi kwa undani unapewa jibu jepesi: "hali ya maisha siyo rafiki (eti-vigumu kwa kijana kuwa na familia) hivyo hawatamani kuoa."

Mtazamo huo hasi unaifanya jamii ipoteze mwelekeo sahihi wa kulitii agizo la Mungu alilowapa 'Adam' na 'Hawa' kwamba "enendeni mkazae, mkaongezeke na kuijaza dunia".

Sipati piacha kamili maana kujitetea kupitia 'ugumu wa maisha' chanzo chake nini?

Ukiuliza wapi umethibitishiwa kimaandishi (au kwa namna yoyote ile) kuwa ulipozaliwa ukahakikishiwa kuwa maisha yako hapa duniani yatakuwa rahisi/mepesi: yaani ule, unywe, uvinjari unavyotaka kirahisirahi bila kutokwa jasho?

Hupata jibu lakini inabaki kulalamikia Serikali na hata wazazi kwa hisia kuwa wanatelekezwa. Wengi malalamiko ni hakuna ajira/kazi. Kwamba fedha imekuwa vigumu kupatikana, na kadhalika na kadhalika!

Ukiwaambia tangu mwanzo binadamu alipomwasi Mungu, kwa mujibu wa maandiko, akaambiwa "kwa jasho lako utakula chakula" mbali ya kuonywa kuwa "asiyetaka kufanyakazi wakati yu mzima wa afya asile chakula".

Sasa huo urahisi wa maisha unaingiaje kama siyo kujidanganya na kupelekea kupenya kwa 'roho' haribifu hatimaye kuukumbatia 'uovu' kwa kutaka kujirahisishia maisha?

Mwanamume simama kidete, fanyakazi kwa bidii ili uitwe baba wa familia na siyo kinyume chake. Kutaka vya urahisirahisi ni kujidhalilisha na kutothaminiwa vizuri na jamii yako.

Na kimsingi ukishaazisha familia, mazingira yatakulazimisha tu kufanya kazi kwa bidii.

Hii ni kukwepa wajibu wa msingi ambao unatutaka wanaume tufanyekazi kwa malengo maalumu ili kuifanya Tanzania kuwa na familia lakini pia nchi ikawa na watu wa kutosha.

Tukumbuke kuwa 'watu/wananchi' ni mtaji muhimu unaohitajika kwa maendeleo ya taifa letu.

Bila watu wa kutosha tunajidanganya na kweli haimo ndani mwetu wakati nchi yetu ni kubwa na idadi ya watu ni ndogo. Ingawa maeneo mengine hayawezi kukaliwa na watu kama sehemu za ardhioevu/maji na hifadhi za wanyama na misitu; bado idadi ya watu ni ndogo.

Takwimu za Sensa ya Watu na Makazi (2022) zinaonyesha kuwa idadi ya watu kwa kilometa moja ya mraba (km2) ni 68 (wastani). Hata hivyo ipo mikoa ambayo watu bado kidogo kama Katavi (watu 25) kwa km2 au Lindi (watu 18) kwa km2 na Ruvuma (watu 29) kilometa moja ya mraba.

Wakati huo tunatarajia kufikia idadi ya watu (Tanzania Bara) 147 millioni (mwaka 2050) kutoka milioni kama 60 ya sasa, sawa na ongezeko la takribani asilimia 3.2 kwa mwaka.

Kwa mwelekeo huu wa 'ushoga/usagaji' kushamiri na vijana wengi kuhofia ndoa kwa visingizio kadhaa; idadi hiyo itatoka wapi? Labda wahamiaji kutoka nje!!!

Pamoja na hayo, vijana wetu wa kiume wamekuwa wepesi kukiuka misingi ya 'ubaba' kupitia familia: 'mume/mke' kuishi pamoja na kupitia baraka ya watoto watakaowazaa wakaitwa 'baba/mama' wa familia na siyo kinyume chake.

Unajiuliza kijana 'mtanashati' na mwenye afya njema anachangamkia "ushoga" na kuona fahari akitangazwa 'shoga'.



Inawezekana akafanya hivyo kwa tamaa ya kupata fedha za haraka kwa kurubuniwa na wenye nia mbaya na kwa kukosa maarifa ya kimbingu anatumbukia kirahisi kwenye mtego wa aina hiyo.

Lakini mapato ya aina hiyo yanafaida gani iwapo hutakuwa na familia na kajivunia uwepo wako katika dunia hii kama dume la mbegu?

Hata hivyo, tukumbuke Mungu tunayemwamini na aliyehai milele yote, yeye ndiye muasisi wa yote: Alfa na Omega. Hakuna wa kulinganishwa naye maana yeye ndiye msingi wa yote yaliyo mema kwa maisha ya binadamu.

Tukumbuke Mwenyezi Mungu hututakia mema kila wakati. Hivyo vijana wetu walijue hilo na wamche Mungu ipasavyo bila shuruti maana kumcha Mungu ni chanzo cha 'maarifa'; ambayo ndiyo hazina kubwa kwa mafanikio yetu la sivyo vijana wengi 'wataangamia' kama Neno la Mungu linavyotuonya: "watu wangu wanaangamia kwa kukosa maarifa".

Vijana kumbukeni ushoga ni dimbwi kubwa la uovu. Ni kinyaa na chukizo kubwa kwa muumba wako. Vilevile, ni kuwa na mioyo iliyosheheni mawazo mabaya na kujivika miguu iliyo miepesi kukimbilia 'maovu'.

Vijana kutumbukia kwenye maovu kama ushoga au usagaji na kwa kisingizio cha 'haki za binadamu' ni sawa na kukosa maarifa hali inayopelekea maumivu makubwa kwa wazazi na jamii kwa ujumla.

Najiuliza wazazi wa kijana kama huyo wanajisikiaje? Wanaposikia au kumshuhudia kijana waliompata akiwa zawadi kutoka kwa Mwenyezi Mungu, ghafla anageuka kuwa mwovu wa kufanya mambo yanayomchukiza muumba na ambayo ni mwiko kwetu sisi Waafrika.

Hebu jiulize. Umezaliwa ni mwanamume iweje uwe na matamanio ya kumuoa mwanamume mwenzako? Iweje, uone fahari na kujisifu kuwa umeolewa na mwanamume mwenzako na kujiona ni mke wake? Kwa hali hiyo wazazi tunajisikiaje kuwaona watoto tuliowazaa kwa mapenzi makubwa ya Mungu wanageuka kuwa 'vituko' kwenye jamii tunayoishi tena bila aibu? Binti naye anageuka kuwa mwanamume eti anamuoa binti mwenzake. Uhalali huo unatokana na nini? Kama jamii tulikatae hili kwa nguvu zetu zote na kulipiga vita. Hakuna cha haki za binadanu wala chochote kile ni 'UOVU' mkubwa.

Kwa hili viongozi wetu wa 'kiroho' kupitia madhehebu mbalimbali simameni imara na kukemea kwa nguvu zote na viongozi wenye mamlaka za kidunia katаeni na kemeeni kwa kinywa kipana. Dunia ituelewe hivyo kuwa hatuko tayari kukumbatia uovu kwa ajili ya kutaka kufurahisha watu wengine.

Mwenyezi Mungu aliivumilia Sodoma na Gomora, akiwaonya waache uovu huo lakini wakawa wakaidi mwishowe wakaangamizwa kwa moto.

Sasa tunaishi kwenye Ulimwengu wa 'Rehema' na 'Neema' za Mungu Mwenyezi; ambaye anatuhurumia lakini kutii sauti yake na maagizo yake na kuuacha uovu ni jambo. linalopendeza mbele yake.

Hatuwezi kudumu na kuendeleza uovu kwa sababu 'Neema' ipo hapana!

Lazima vijana wetu waenende katika njia zisizoleta machukizo kwetu wazazi/jamii nanMungu wetu pia.

Vijana wengi wanalia kuwa hali ya uchumi na maisha inakuwa ngumu na ajira ni kidogo kulingana na mahitaji, Kazi za kujituma hata kama ni kulima, kufuga au kazi nyinginezo za kumpatia kijana kipato zinapuuzwa kwa kutaka kupata fedha kirahisirahisi wakati kwa jasho letu; tunapaswa kupata riziki zetu za kila siku.

ukumbuke kwamba inapotokea uovu ukakithiri kwenye jamii milango ya Baraka katika 'Ulimwengu wa Roho' inafungwa. Hatuwezi kumlaumu Mungu kwa sababu tunajiangamiza kwa kukosa maarifa.

*Itaendelea*



Hamisi Kibari

## TUKUBALIANE KUTOKUBALIANA

Simu: 0758143457

# Sukari imeshuka bei, Chadema mna nyimbo nyingine?

"SASA hivi wamekuja na ajenda nyingine, hali ngumu ya maisha... Kwani wana CCM hawaguswi na ugumu wa maisha. Rais Samia Suluhu Hassan mwaka jana aliwekeza bilioni 100 kila mwezi kukabiliana na bei ya mafuta, mbona hili hawalisemi?"

Hiyo ni kauli iliyotolewa hivi karibuni na Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Abdulrahman Kinana alipozungumzia kuvunjika kwa mazungumzo ya maridhiano baina ya CCM na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA).

Kimsingi, Kinana alisema moja ya sababu ya kuvunjika kwa mazungumzo hayo ni kuchoshwa na tabia ya Chadema ya kutotumia lugha za staha kwa kiongozi na Mkuu wa nchi wanapokuwa kwenye mikutano yao.

Lakini pia akawa anahoji Chadema wanachokitaka ni nini hasa? Dira yao nini. Sera mbadala zao ni zipi? Ndipo akasema:

"Chadema hawaeleweki wanataka nini. Hapohapo wanaandamana, hapohapo walipeleka watu bungeni kutoa maoni yao, hapohapo wanataka maboresho ya sheria, hapohapo wanaandamana kupinga muswada wa sheria, hawaeleweki wanataka nini," alisema Kinana.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Prof Kitila Mkumbo ambaye ametokea upinzani aliwahi kusema kwamba upinzani unaweza kujikuta katika wakati mgumu usipokuwa na hoja na mbinu za kushindana na Serikali na badala yake wakabaki kwenye mazoea ya kusubiri CCM wakosee ndo wapate hoja!

Pamoja onyo hilo la Profesa Mkumbo na hata wale walioandika ulioitwa mkakati wa mabadiliko ndani ya Chadema na kujikuta wamefukuzwa, waliwahi kukionya chama hicho kubadili mwenendo wake.

Hata hivyo, imekuwa sawa na kumpigia mbuzi gitaa. Chadema imeendelea kuonesha kwamba ni chama cha siasa za matukio na 'kuokoteza' yale yanayoonekana kuwa mapungufu ya serikali ili kupata cha kusema kwa watu kikiamini kwamba kwa hatua hiyo labda kitajiongezea wanachama.

Katika 'kuokoteza' huko, hivi karibuni, Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe aliibuka na na jambo la ajabu aliposema:

"Wabunge walikuwa na mshahara wa shilingi milioni 13 wakati natoka bungeni. Bunge ambalo limejaa wabunge wa CCM mwaka 2023 wakajiongezea mshahara hadi Sh milioni 18, hebu fikiria manesi, walimu na madaktari wetu wanalipwa nini, mshahara hautoshi."

Kabla ya kuijadili kauli hii, ieleweke kwamba imekanushwa tayari na Ofisi ya Bunge, hali inayodhihirisha sifa nyingine ya Chadema ya kuokoteza habari kwenye korido na kuzifanya mtaji wa kiasasa bila hata kuzifanyia kazi kwa kina ili kujua ukweli wake.

Hii iliwahi pia kuwagharimu baadhi ya viongozi wa Chadema kushtakiwa na kushindwa kutoa ushahidi wa madai waliotoa dhidi ya viongozi. Ni kama Chadema wameshindwa kusoma mazingira ukutani kwamba zama zimebadilika. Ukizuka na jambo usilo nalo ushahidi na hasa kama linamhusu mtu binafsi, basi ujue mtakutana mahakamani.

Ningali ninajiuliza kwamba hivi kweli Mbowe ni mtu wa kushindwa kupata usahihi wa mishahara ya wabunge kabla ya kwenda 'kuruka na udaku'.

Lakini sasa tuje kwenye hoja ya Mbowe. Hivi shilingi milioni 13 ni nyingi au chache? Ni nyingi au chache kwa nani? Shilingi milioni 18 je?

Kwa wengine, shilingi milioni 13 pia ni nyingi sana lakini la kujiuliza wakati akiwa bungeni Mbowe aliziona chache? Hazikuwa nyingi kuwafikiria manesi, polisi, walimu na madaktari au hawakuwepo. Je, haya mapenzi ya ghafla kwa wananchi yamekuja je?

Lakini hata kama wabunge wangepandishiwa mishahara na kufikia hizo shilingi milioni 18, bila shaka hazipandi hivihivi bali zinategemea mazingira, vigezo na hali ya uchumi wa nchi. Tukubali tusikubali wabunge ni wawakilishi wetu na wana majukumu mengi na muhimu.

Wabunge ni watu wanaoishi na wananchi na kwa kweli wengi wao naweza kusema ni kama mashine za kutolea pesa (ATM) za wananchi. Walio wengi, tunawaona kwenye kusaidia wapiga kura wao katika masuala mbalimbali kama misiba hadi kusaidia karo za shule.

Ninajua hii si kazi ya wabunge lakini wao ni watumishi wa wananchi kwa hiyo mara nyingi mazingira yanawafanya kujikuta katika hali ya kulazimika kuingia kwenye mifuko yao kusaidia kero mbalimbali za wananchi.

Tumeshuhudia pia baadhi ya wabunge wakishindwa hata kulipa madeni kutokana na matumizi mengi ya pesa wanayolazimika kuyafanya.


Lakini hii Chadema ya Mbowe kweli ina 'moral authority' ya kuzungumzia mishahara ya wafanyakazi? Si ndio chama hiki kinawakataa wabunge wake wa viti maalumu bungeni, akina Mdee na kundi lake wakati huohuo wameomba pesa za ruzuku za wabunge hao zipatazo bilioni mbili.

Kwa nini hawajasema pesa hizo, kwa kuwa hawawatambui akina Mdee, zigawiwe kwa wafanyakazi ama kufanya kazi nyingine za kijamii?

Ukisoma ule Mkakati wa Mabadiliko ulioandikwa mwaka 2013, ulionesha kwamba uongozi wa akina Mbowe ni wabadhirifu ajabu. Hawa ndio wanaweza kuwa watetezi wa mishahara ya wafanakazi?

Lakini tutoke huko, tuje sasa kwenye maandamano ya Chadema ambayo hivi karibuni Mbowe alikaririwa akisema sasa yatakuwa mithili ya mila.

Maandamano yao, mwanzo yalikuwa kama ya upinga baadhia ya miswada iliyokuwa ikipelekwa bungeni.



**Chadema hawaeleweki wanataka nini. Hapohapo wanaandamana, hapohapo walipeleka watu bungeni kutoa maoni yao, hapohapo wanataka maboresho ya sheria, hapohapo wanaandamana kupinga muswada wa sheria...**

Lakini ghafla tukaanza kusikia mwelekeo wa maandamano yao ni kuzungumzia ugumu wa maisha na hususani wakijikita kwenye sukari ambayo kimsingi serikali ilijitahidi kueleza sababu ya uhaba wa sukari na kusababisha bidhaa hiyo kupanda.

Baadhi ya sababu zilielezwa kwamba ni kutokana na madhara ya mvua nyingi yaliyopelekea kupungua kwa uzalishaji.

Leo bei ya sukari mijini hadi vijijini imeshuka. Kilo ni wastani wa Sh. 3200 na inasema bei inakwenda kushuka zaidi mpaka 2,500.

Kimsingi, ukiachana na sukari, gharama ya bidhaa nyingi zimeshuka lakini hili Chadema hawalioni na wala hawazungumzii namna serikali ilivyoweka ruzuku kwenye mbolea.

Nimalizie kwa kuwaomba Chadema waache kuwa chama cha matukio. Ili kukiokoa chama hicho, viongozi waliopo wakubali kwamba wamechoka, waachie wengine kukiongoza kwa sababu maandamano hayawezi kuwafikisha kokote.

Kwenye mkakati wa mabadiliko iliandikwa namna hii. "Ni dhahiri mabadiliko (ya uongozi) yanahitajika kwa kuwa wakuu waliopo wanatumia mbinu zilezile na kupata matokeo yale yale."

Chadema pia ifanyie kazi maneno haya ya Waziri Mkumbo aliposema kwamba wapinzani hawawezi kushika Dola kwa kuwa mabingwa wa kukosoa badala ya kuja na sera mbadala.

Haya, la kupanda mishahara ya wabunge limekanushwa na sukari imeshuka, sasa tunasubiri wimbo ambao Chadema Jazz Band mtakuja nao.

# Dk. Samia anavyowaumbua wapinzani uchwara!

## ● Anatenda bila jazba, siyo mwoga na anamudu vishindo



**Na Hamid Yassin**

VIONGOZI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) wanaendelea kuzunguka mikoa kadhaa kujaribu kumchafua Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, Serikali yake sambamba na Chama tawala (CCM), lakini sasa wanaumbuliwa na mapokeo ya miaka yake mitatu madarakani.

Kila pembe Tanzania sasa inamwimba Mama Dk. Samia kwa mazuri zaidi kuliko yale mabaya ya kupikwa dhidi yake.

Machi 19 wiki iliyopita Rais Dk. Samia ametimiza miaka mitatu ya mafanikio ya kutukuka madarakani, huku baadhi ya viongozi wa vyama vya upinzani aliowatoa jela ya kisiasa ya miaka sita wakiumbuka hadharani baada ya kupambana kuviza na kufisha hatua kubwa ya maendeleo yaliyoletwa hapa nchini na Serikali hii ya Awamu ya Sita.

Awali Mwenyekiti wa chama hicho kikuu cha upinzani, Freeman Mbowe na wenzake walitoa sifa kemkem kwa Rais Samia lakini sasa katika hali ya kushangaza wamegeuka kama kinyonga na kupambana 'kumsagia kunguni' kwa wananchi kupitia maandamano yao waliyofanya kwenye mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Mbeya na Arusha! Lakini wapi, Mama hachafuliki!

Kupitia moja ya zile 'R' zake nne katika kipindi hiki cha uongozi wake, alitumia ile ya Maridhiano (Reconciliation), kukutana na viongozi wa vyama vya upinzani na kufanya nao mazungumzo yenye lengo la kujenga na kuleta maridhiano na umoja wa kisiasa nchini.

Miongoni mwa viongozi aliokutana nao ni pamoja na Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe mara tu baada ya kutoka mahabusi mwaka 2021 alikokuwa rumande akikabiliwa na kesi.

Pia Rais kwa nyakati tofauti alikutana na viongozi wa vyama vya ACT Wazalendo, Chama cha ADC, Chama cha Wananchi (CUF) na pia viongozi wa Kituo cha Demokrasia Tanzania (TCD)

Katika mikutano yote hiyo, Dk. Samia alikuwa akisisitiza umuhimu wa kushirikiana ili kuijenga Tanzania ya kuaminiana na kuheshimiana kwa misingi ya haki na kusahau yaliyopita.

Akizungumza kuhusu suala la maridhiano mara baada ya kukutana na Dk. Samia, Mwenyekiti wa Chadema, Mbowe alielezea umuhimu wa kuondoa uhasama wa kisiasa pamoja na kusameheana.

"Ameonesha njia kwa taifa letu namna tunavyopaswa kuwa, Rais Samia na Falsafa yake ya R nne katika kuijenga nchi yetu Tanzania amedhamiria kusameheana ili kwa pamoja tujenge taifa lenye uhuru, haki, demokrasia, na maendeleo ya watu wote," alinena Mbowe bila kupepesa macho wala mdomo ingawa sasa amekuwa tofauti.

**MWENYEKITI ADC AWASHANGAA**

Mwenyekiti wa Chama cha Alliance for Democratic Change (ADC), Hamad Rashid Mohamed amewashangaa wapinzani wenzake kwa madai yao kwamba Dk. Samia anaminya demokrasia hapa nchini na kubainisha kwamba si kweli hata kidogo.

Akizungumzia miaka mitatu ya awamu ya sita, Hamad ameweka wazi kuwa, Serikali hii imefanya mambo mengi mazuri katika kipindi hiki kifupi kama vile kuruhusu siasa kufanyika kwa uhuru mkubwa kulinganisha na awamu iliyopita.

"Nadhani hawa wenzetu wana ajenda yao ya siri au wameamua tu kuvaa miwani ya mbao kwa makusudi ili wasione haya maendeleo yanayofanywa na awamu hii ya sita chini ya Dk. Samia," ametanabahisha Hamad Rashidi.

Mwanasiasa huyo mkongwe aliyetokea CCM kisha kwenda kuasisi Chama cha upinzani cha Wananchi (CUF) na wenzake akiwemo Hayati Seif Sharif Hamad, marehemu Shaban Khamis Mloo na wengineo kabla ya kutofautiana na kuibukia ADC, amesema mnyonge anyongwe lakini haki yake apewe; akifafanua kwamba akina Mbowe hawamtendei haki Rais Samia.

Kiongozi huyu ambaye ameshashika nyadhifa kadhaa kubwa kwenye Serikali ya Muungano na ile ya Zanzibar ikiwemo ile ya maridhiano chini ya marais wastaafu, Amani Abeid na Dk. Mohamed Shein, amewapasha viongozi wa Chadema kwamba hata yale majukwaa wanayotumia 'kumnanga' Dk. Samia ni yeye aliyeruhusu!

"Serikali ya awamu ya tano iliweka msimamo wake kwamba uchaguzi ukiisha watu wakafanye kazi, hakuna cha kufanya siasa, mikutano ya ndani wala ya hadhara. Sasa Rais Samia amewarejeshea haki yao ya kikatiba badala ya kumpongeza wao wanazurura mikoani wakimlaumu!" Ameshangaa Hamad Rashid.

Ameongeza kwamba kilio kikubwa kule kambi ya upinzani kilikuwa ni mabadiliko ya Katiba ambayo Dk. Samia aliunda Sekretarieti Maalumu iliyozunguka nchi nzima na kusikiliza maoni toka wananchi wa kada mbalimbali



wakiwemo viongozi wa vyama vyote vya siasa na wale wa taasisi za dini na wananchi uliokuwa ukiratibiwa na ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa na Baraza la Vyama vya Siasa ili kupitia miswada ya marekebisho ya katiba.

Miswada iliyopitishwa na Bunge anayoizungumzia Hamad Rashid ni pamoja na ule wa Sheria ya Uchaguzi ya Rais, Wabunge na Madiwani ya mwaka 2023, Muswada wa Sheria ya Tume ya Uchaguzi wa mwaka 2023 na Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Vyama vya Siasa wa mwaka 2023. Hii ilipingwa na Chadema na walitaka itolewe Bungeni.

Tangu wiki iliyopita vyombo mbalimbali vya habari, wizara, idara za Serikali na taasisi tafauti zimekuwa zikiweka hadharani mambo yote ya maendeleo yaliyofanywa katika hii miaka mitatu ya awamu ya sita; hivyo nachelea kuandika hayo yote kwani nitakuwa narudia tu hapa na karibu kila sekta kumekuwa na mabadiliko chanya.

Ndiyo maana makala haya yamejikita zaidi katika kuwashangaa wale wanaojifanya hawazioni kazi hizo na hayo maendeleo yaliyoletwa na awamu hii chini ya Dk. Samia hususani baadhi ya vyama vya siasa vya upinzani wakiongozwa na kinara wao Chadema.

**DK. SAMIA NI NANI?**

Samia Suluhu Hassan alizaliwa Januari 27 mwaka 1960. ni Rais wa Sita wa Tanzania. Kabla ya kuwa rais kutokana na kifo cha John Magufuli, kilichotokea tarehe 17 Machi 2021, Samia alikuwa Makamu wa Rais kwa sababu ya kuwa mgombea mwenza katika Uchaguzi Mkuu wa 2015 na kisha uchaguzi wa 2020.

Alisoma shule za msingi za Chwaka hapo Unguja, Ziwani kule Pemba na Mahonda (Unguja) katika miaka ya 1966 hadi 1972. Aliendelea na masomo ya sekondari shule za Ng'ambo, Unguja (1973-1975) na Lumumba, Unguja (1976).

Baada ya kumaliza masomo yake ya sekondari mnamo 1977, aliajiriwa na Wizara ya Mipango na Maendeleo kama karani. Alisoma kozi fupi kadhaa. Mnamo 1986, alihitimu diploma ya juu katika utawala wa umma kutoka Taasisi ya Usimamizi wa Maendeleo (sasa Chuo Kikuu cha Mzumbe ).

Baada ya kuhitimu, aliajiriwa kwenye mradi uliofadhiliwa na Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (World Food Programme). Kati ya mwaka 1992 na 1994, alisoma kwenye Chuo Kikuu cha Manchester, Uingereza na kuhitimu stashahada ya uzamili katika uchumi.

Mwaka 2000 aliamua kujiunga na siasa. Aliteuliwa na CCM kama mbunge wa viti maalumu katika Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, akateuliwa na Rais Amani Karume kuwa Waziri wa Utalii na Bishara. Alichaguliwa tena mnamo 2005 kwenye viti maalumu na aliteuliwa tena kama Waziri katika Wizara ya Kazi, Jinsia na Watoto.

Mwaka 2010 aligombea kwenye uchaguzi wa Bunge la Kitaifa, akisimama katika jimbo la Makunduchi na kushinda kwa zaidi ya asilimia 80. Rais Jakaya Kikwete alimteua kuwa Waziri wa Nchi katika ofisi ya Makamu wa Rais anayeshughulikia Mambo ya Muungano.

Mwaka 2014 alichaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalumu la Katiba lililokuwa na jukumu la kuandaa katiba mpya ya nchi.

Mnamo mwaka 2015, alipata shahada yake ya pili (MSc) katika Maendeleo ya Uchumi wa Jamii kupitia mpango wa pamoja kati ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania na Chuo Kikuu cha Kusini mwa New Hampshire.

Makamu wa Rais

Mnamo Julai 2015, mteule wa urais wa CCM, John Magufuli alimchagua kuwa mgombea mwenza wa uchaguzi wa 2015 na kumfanya kuwa mgombea mwenza wa kwanza mwanamke katika historia ya chama hicho. Baadaye alikuwa Makamu wa Rais wa kwanza mwanamke katika historia ya nchi kutokana na ushindi wa Magufuli katika uchaguzi ule.

Novemba 5 mwaka 2015 aliapishwa kama Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akiwa mwanamke wa kwanza kufikia cheo hicho, akarudia baada ya uchaguzi mkuu wa tarehe 29 Oktoba 2020.

**URAIS**

Sasa amekuwa rais wa kwanza mwanamke na rais wa pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutoka Zanzibar, wa kwanza alikuwa hayati Ally Hassan Mwinyi, Rais wa awamu ya Pili.

Dk. Samia aliingia madarakani Machi 19 mwaka 2021 kutokana na utaratibu wa Katiba ya nchi kufuatia kifo cha mtangulizi wake, hayati John Magufuli.

Aprili 30 mwaka 2021 alichaguliwa kuwa Mwenyekiti wa CCM akiwa mwenyekiti wa kwanza mwanamke.

Wanazengwe walikuwa na wasiwasi naye, lakini Dk. Samia ameonesha ni mtulivu na mtu makini na hicho ndicho kipimo cha busara kwa mujibu wa maandiko. Dk. Samia siyo mama amri. Akihutubia hana vishindo wala msisitizo wa ubabe kwamba yeye ni Rais.

Dk. Samia hapayuki, hadhalilishi wa chini yake kwa maneno mabaya. hainui mabega kwamba yeye ni mwanamke wa kwanza kuwa na cheo kikubwa kuwahi kutokea nchini. Daima huvaa nafasi mbili, kama mwanamke mlezi wa wana na kama kiongozi mwenye madaraka.

Tangu Machi 19 2021, alipokula kiapo cha utii na uaminifu kuwa Rais, Dk. Samia hajawahi kusikika akifoka na kusema "mimi ndiye Rais", hajasema; huku ukweli ukiwa wazi kwamba yeye ndiye Rais pekee mwanamke wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwahi kutokea!

Ni kwa kutambua hivyo ndiyo maana humuoni Dk. Samia mwenye mihemko. Bali Watanzania wanamshuhudia Rais wao mwenye lugha laini, zenye kuonya panapostahili kuonya na kutoa maelekezo mahsusi mahali ambapo yanahitajika.

Thamani kubwa zaidi kwa Dk. Samia ni nidhamu. Aliwahi kuwaambia wanawake kutambua nafasi zao. Akasema kuwa yeye pamoja na kuwa ni Rais lakini akifika nyumbani anampigia goti mume wake.

Dk. Samia alisema kuwa utamaduni wa Mtanzania lazima uendelezwe kwa wanawake kuwa watiifu kwa waume zao. Akajipambanua yeye binafsi kama mfano. Ana madaraka makubwa serikalini, cheo namba moja kwenye nchi lakini hajapoteza utiifu kwa familia yake wala jamii ya Watanzania.

Jinsi alivyoonesha utulivu na busara wakati wa Bunge la Katiba mwaka 2014 alipokuwa Makamu Mwenyekiti, ilitosha kumpambanua kuwa mwanamke wa aina gani. Mama yetu hutenda mambo yake bila jazba halafu siyo mwoga na anamudu vishindo vya wenye kuzua vishindo.

Muone sasa Dk. Samia; ni mtulivu na mpole lakini mwanamke imara sana anapokabiliana na watu wenye vishindo.

Basi tu baadhi ya viongozi wa vyama vya upinzani wanakosa fadhila kwa kutaka kumchafua wakati yeye ndiye amewatoa kwenye 'jela' ya kisiasa ya takribani miaka sita!

Uzuri wa Dk. Samia ni kwamba anapokabiliana na watu wakorofi wala yeye hapayuki. Anakupa nafasi uoneshe ungangari wako kisha anakudhibiti bila kelele. Halafu wewe uliyedhani ni imara, mwenyewe unajikosoa kwamba umekutana na mwanamke imara zaidi.

Ombi langu kwa Watanzania wenzangu, kwa hiki alichotuonyesha Mhe. Dk. Samia hatuna cha kumlipa zaidi ya kumrudisha madarakani kwenye Uchaguzi Mkuu ujao wa mwakani 2025.

Kumrudisha? Ndiyo; Machi 19 mwaka 2021 aliapishwa kuwa Rais wa Tanzania kwa mujibu wa Katiba ya nchi. Hatukumweka sisi, safari hii ni zamu yetu. Mwenyezi Mungu akituweka hai tumrudishe Ikulu kwa njia ya sanduku la kura! Inshallah.

***Kwa maoni; 0768 888 787 ama 0784 122020.***



# VETA inavyounga mkono upandaji miti miaka 60 ya Muungano

**Na Mwandishi Wetu**

Upandaji miti unatajwa miongoni mwa njia muhimu za kukabiliana na changamoto ya mabadiliko ya tabianchi inayoikabili jamii yetu na Dunia kwa ujumla.

Wataalamu wa mazingira wanashauri upandaji miti kwa wingi kama njia mojawapo ya kuboresha mazingira na kuokoa maisha ya viumbe hai ikiwemo binadamu. Ndiyo maana Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeendelea kuweka msisitizo kwa wananchi wake kupanda miti.

Januari 25, 2024, Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) ilizindua zoezi la upandaji miti kuelekea Maadhimisho ya Miaka 60 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dkt. Selemani Jafo, alisema zoezi hilo ni mwendelezo wa kampeni ya Serikali ya uhifadhi wa mazingira hususani, kupanda na kutunza miti. Dkt. Jafo alisisitiza kila mwananchi kupanda mti wa kumbukumbu ya Muungano na kila taasisi katika ngazi zote, kitaifa, kimkoa na mamlaka za Serikali za Mitaa, kupanda miti isiyopungua 60 kama alama ya miaka 60.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan aliadhimisha siku ya kumbukumbu ya kuzaliwa kwake Januari 27, 2024 kwa kuungana na wananchi wa makundi mbalimbali kupanda miti 4720 ikiwemo miti 120 ya matunda katika eneo la Donge Muwanda, visiwani Zanzibar.

Rais Samia aliadhimisha siku hiyo kwa kupanda miti kwa sababu ya kuwepo kwa uharibifu mkubwa wa mazingira nchini hasa visiwani humo na kusema kuwa upandaji wa miti kwa wingi utasaidia kurudisha hali asilia ya bahari na kupunguza kasi ya mmomonyoko wa ardhi.

Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA), imeitikia wito huo na kuanza utekelezaji wake ambapo hadi sasa miti zaidi ya 40,000 imepandwa na watumishi na wanafunzi wa mamlaka hiyo.

Akizungumza wakati wa zoezi la upandaji miti lililohusisha watumishi wa VETA Makao Makuu jijini Dodoma tarehe 25 Machi, 2024, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa VETA, CPA Anthony Kasore, amesema zoezi hilo limefanyika kwenye vituo vya VETA nchini ikiwa ni utekelezaji wa maagizo ya Serikali ya kila mwananchi na kila taasisi kupanda miti ili kutunza mazingira.

Katika Chuo cha VETA Wilaya ya Bahi mkoani Dodoma, jumla ya miti 700 imepandwa katika eneo la chuo hicho ikiwa ni hatua ya kutunza mazingira. Zoezi la upandaji miti chuoni hapo lilizinduliwa na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule tarehe 20 Februari, 2024 na kuhusisha viongozi mbalimbali wa Wilaya hiyo pamoja na walimu na wanafunzi wa VETA Bahi.

Senyamule alisisitiza utunzwaji wa chuo hicho ikiwemo miche iliyopandwa ili ikue na kuleta mandhari nzuri ya chuo na hatimaye kuweka mazingira mazuri ya kufundishia na kujifunzia.

Kaimu Msajili wa Chuo cha VETA Wilaya ya Bahi, Daudi Lyanga anasema wanafunzi wanashiriki vyema katika utunzaji wa miche iliyopandwa na kwamba wamekuwa wakipata elimu mara kwa mara juu ya umuhimu wa kutunza mazingira.

Maofisa misitu wameendelea kututembelea na kutoa elimu kwa wanafunzi wetu juu ya utunzaji wa mazingira na wanafunzi wetu wanafurahia kufanya shughuli mbalimbali kama vile kumwagilia miche ya miti na kuandaa bustani za mbogamboga na matunda, amesema

Februari 28, 2024, Mkuu wa Wilaya ya Uyui, Zakaria Mwansasu aliongoza zoezi la upandaji miti katika chuo cha VETA Wilaya ya Uyui, mkoani Tabora. Walimu na wanafunzi wa chuo hicho walishiriki katika zoezi hilo ambapo miche ya miti 500 ilipandwa katika maeneo mbalimbali ya chuo.

Akizungumza baada ya zoezi la upandaji miti, Mwansasu alisisitiza miti hiyo kutunzwa na kuagiza kila mwanafunzi chuoni hapo kukabidhiwa mti kwa ajili ya kuutunza.

Nakabidhi miti hii naomba kila shimo liwe na mwanafunzi mmoja au wawili ili huo mti ukipotea au kukauka ni lazima urudishiwe. Tusipande miti halafu kesho na keshokutwa miti hiyo inakauka, alisema.

Naye Kaimu Msajili wa chuo hicho, Fedric Lukumay aliahidi kusimamia utunzaji wa miti hiyo pamoja na mazingira ya chuo ili kufanya madhari ya chuo hicho kuwa mazuri.

Kasore amewaasa watumishi na wanafunzi kutunza miti iliyopandwa ili ikue na kuleta maana halisi ya zoezi hilo na pia amewahimiza watumishi kuendelea na zoezi hilo katika maeneo wanayoishi.

Kupanda miti ni jambo moja na kutunza miti hiyo ni jambo lingine la muhimu sana Nasisitiza tukatunze miti hii ili ikue na kutupa uhai pamoja na kuboresha muonekano wa mazingira yetu, amesema.

Kasore ameshukuru Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) kwa kutoa miti hiyo bure na kuahidi kuendeleza ushirikiano katika shughuli mbalimbali za uhifadhi wa misitu na utunzaji mazingira.

Afisa Misitu wa TFS Kanda ya Kati, Jenipha Elius, aliyesimamia zoezi la upandaji miti kwa watumishi wa VETA Makao Makuu, amesema anaamini miti hiyo itatunzwa na kukua vizuri hasa kwa kuzingatia kuwa imefuata hatua zote muhimu za kitaalamu za upandaji miti.



Amewasihi watumishi wa VETA kujenga utamaduni wa kupanda miti kwenye maeneo wanayoishi na kujipatia faida mbalimbali ikiwemo hali nzuri ya hewa pamoja na matunda na kuwakaribisha kupata miti bure kutoka TFS.

Furaha Paul ni miongoni mwa watumishi wa VETA Makao Makuu walioshiriki zoezi hilo ambaye amesema amejisikia fahari kupanda miti ambayo itanufaisha watanzania wengi kwa miaka mingi ijayo.

Kwa kweli najisikia furaha kushiriki kwenye zoezi hili la kihistoria kwa kuwa naamini miti hii itatumiwa na sisi, watoto wetu, wajukuu hadi vitukuu vyetu, amesema

Kilele cha Maadhimisho ya Miaka 60 Muungano wa Tanganyika na Zanzibar kinatarajiwa kuwa Aprili 26, 2024.

# Baadhi ya mambo muhimu kujua mwezi wa Ramadhani

**Na Mwandishi Wetu**

Waislamu duniani kote wanaendelea na Mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani na haya ni mambo muhimu ya kujua katika mwezi huu.

**NIA YA KUFUNGA INAPATIKANAJE?**

Wanazuoni wanakubaliana kwamba kujichunga na vitu vinavyoharibu swaumu (pia hutamkwa saumu) kuanzia alfajiri inapoingia hadi magharibi ni nguzo kuu ya funga baada ya mfungaji kuweka nia ya kufunga.

Nia ni ya moyoni mwa mtu na si kutamkishwa na mtu mwingine kama wengi wanavyodhani au kama inavyofanyika kwa baadhi ya watu.

Nia ya kufanga inatakiwa ipatikane kila siku kabla ya kuingia alfajiri. Wanazuoni wanaamini kwamba hata kujiandaa kwa ajili ya daku kwa lengo la kufunga kesho yake ni nia tosha.

Baadhi ya wanazuoni wanaamini pia kwamba ukichukulia Ramadhani nzima kama ibada moja basi ukinuia kufunga mwezi mzima tayari ni nia inayotosha pia.

Kufunga si kujizuia na kula na kunywa pekee bali pia kujizuia na machafu kama vile kusengenya, kusema uongo, kutazama maovu na hata kuyaendea.

**DUA IPI SAHIHI WAKATI WA KUFUTURU?**

Baadhi ya wafungaji wengi wakati wa kufuturu huleta dua ya "Allaahumma laka swumtu wa 'ala rizqika aftartu" (Ewe Mwenyezi Mungu Mlezi, kwa ajili yako nimefunga na kwa riziki ulionipa ninafungua swaumu ya leo)."

Kufuturu kwa kuanza na dua hiyo kunatokana na hadithi dhaifu iliyoelezewa na Abu Dawood (2358) kutoka kwa Mu'aadh ibn Zuhrah, ambaye anasema alimsikia Mtume Muhammad (S.A.W) akisema dua hiyo wakati wa kufuturu.

Hakuna haja ya kutumia dua hii dhaifu kwa sababu kuna ripoti sahihi kutoka kwa Abu Dawood huyo huyo (2357) kutokana na hadith ya Ibn 'Umar (Mwenyezi Mungu awe na radhi naye) ambaye anasema: Wakati Mtume wa Mwenyezi Mungu Mlezi (Amani na Rehema za Mwenyezi Mungu Mlezi ziwe juu yake) akianza kufuturu alikuwa akisema: "Dhahaba al-zamau'a, wa abtallat al-'uruuq wa thabata al-ajr insha Allah (Kiu imeondoka, mishipa ya damu imejaa, na malipo yatapatikana, kama Mwenyezi Mungu Mlezi atataka)." (al-Albaani katika Saheeh Abi Dawood).

Pili, ni muhimu kwa mtu aliyefunga kuomba dua wakati wote ikiwa ni pamoja na wakati wa kufuturu. Hii ni kutokana na mapokezi ya Ahmad (8030) kutokana na hadithi ya Abu Hurayrah ambayo ina meneno mengi lakini inaisha kwa kumkariri Mtume (SAW) akisema: "Kuna watu watatu ambao dua zao hazirejeshwi (bila kupokelewa na Mwenyezi Mungu Mlezi): kiongozi mwadilifu, mtu aliyefunga swaumu hadi anapofuturu, na maombi ya mtu aliyepotezwa..."

Kwa mantiki hiyo mfungaji anatakiwa kumuomba sana Mwenyezi Mungu Mlezi amwingize peponi na kumsamehe makosa yake pamoja na dua zingine kwa maisha ya dunia.

**VITU GANI VINATENGUA SWAUMU?**

Mwenyezi Mungu Mlezi ametupa ibada ya kufunga katika misingi ya busara ya hali ya juu.

Anamtaka mja wake afunge lakini katika mazingara ambayo hayatakuwa sababu ya yeye kudhurika lakini mfungaji hatakiwi kufanya kile ambacho kitaharibu funga yake.

Kwa msingi huo, vitu vinavyoharibu/kubatilisha swaumu vinaweza kugawanyika katika makundi mawili; mosi ni vinavyotoka mwilini kama vile kujitapisha kwa makusudi, kufanya tendo la ndoa mchana wa Ramadhani, kupata damu ya hedhi na kupiga chuku (tiba inayohusisha kutoa damu ama pia inajulikana kama kuumika au hijama -blood cupping).

Vitu hivi vinapotoka ndani ya mwili huufanya kuwa dhaifu. Kwa mantiki hiyo Mwenyezi Mungu Mlezi amevieleza kama vitu vinavyotengua swaumu.

Aina ya pili ya vitu vinavyoharibu saumu ni vile vinavyoingia kwenye mwili wa binadamu kama vile kula na kunywa. Kama mtu atakula na kunywa hatofikia lengo la kufunga.

Mwenyezi Mungu katika al-Baqarah 2:187 ametaja vitu vitatu vinavyotengua saumu; kula, kunywa na kufanya tendo la ndoa. Vitu vingine vinavyotengua swaumu vimetajwa na Mtume (SAW) kupitia hadithi zake (matamshi, matendo ama yale yaliyofanywa mbele yake akayaridhia ama kuyakataza).

**MAMBO SABA YANAYOTENGUA SWAUMU**

Kwa ushahidi wa Qur'an na hadith hizo wanazuoni wametaja mambo saba yanayotengua swaumu ambayo ni: kufanya tendo la ndoa mchana wa Ramadhani, kujichua hadi kutoa manii, kupatwa hedhi (kwa akina mama) au damu ya uzazi (nifaas), kula na kunywa, chochote kinachoweza kuchukuliwa kama "kula na kunywa", kutoa damu kwa njia ya hijama ama yanayofanana na hayo na kutapika kwa makusudi.

**UFAFANUZI ZAIDI**

Kufanya tendo la ndoa mchana wa Ramadhani ni kosa kubwa kwa mfungaji. Hapa ni pale tupu



mbili zinapokutana hata kama mshindo haukutokea, watu hao wanakuwa wametengua funga yao. Licha ya kwamba hawatotakiwa kula isipokuwa kumalizia siku, wanakabiliwa na kufanya kafara kubwa.

Wakati anayefungua kwa sababu sita zilizobaki analipa siku alizokosa peke yake, mwenye kufanya tendo la ndoa na mkewe mchana wa Ramadhani anatakiwa kulipa kwa kufunga siku 60 au kulisha maskini 60 ama kumwachia mtumwa huru kama anaye.

Ufafanuzi kuhusu kujichua kwa kutumia mkono hadi kufikia mshindo (masturbation) kunaelezwa kuwa, mbali ya kuwa kitendo hicho ni haramu, pia kinatengua saumu ya mfungaji.

Wanazuoni wanakubaliana kwamba kama mtu ataanza kujichua kisha akaacha bila kufikia mshindo, anapaswa kuleta toba kwa kosa hilo lakini funga yake itakuwa haijatenguka.

Mtu aliyefunga anapaswa kujiweka mbali na mambo yanayotamanisha kama vile kutoangalia watu waliovaa nusu uchi, picha za utupu na asikaribishe mawazo yanayoweza kumfanya atamani kufanya tendo la ndoa ama kujichua.

Kuhusu mtu kutokwa na madhii (majimaji ambayo si manii), wanazuoni walio wengi wanakubaliana kwamba hayatengui saumu ya mtu.

Kifunguzi cha tatu, kula na kunywa, wanazuoni wanafafanua kwamba ni chochote kitakachofika tumboni kupitia mdomoni.

Kuhusu yale yanayoingia pia kwenye kichwa cha habari 'kula na kunywa' yanahusisha mambo yafuatayo:

Mosi, ni kuongezewa damu kwa mtu ambaye anafunga. Hili linabatilishwa swaumu kwani damu inatokana na chakula na vinywaji.

Pili, ni kulishwa chakula ama kitu mbadala wa chakula kwa njia ya mpira ama dripu. (Fatwa ya Shekhe Ibn Uthaymeen katika Majaalis Shahr Ramadhaan uk 70).

**SINDANO HAIHARIBU SWAUMU**

Kuhusu sindano ambayo mtu hachomwi kwa ajili ya kuwa mbadala wa chakula ama kinywaji isipokuwa kwa ajili ya tiba ama chanjo, yaani kama vile sinadano ya kutibu maleria ama insulini kwa ajili ya kisukari havitengui swaumu hata kama zinachomwa kwenye mishipa ya damu.

Hata hivyo, katika kuwa katika hali ya usalama zaidi inashauriwa kwamba ni vyema sindano mtu akachoma usiku.

Kusafishwa figo (Kidney dialysis) ambapo mgonjwa huongezewa kemikali fulani na sukari wanazuoni wengi wanakubaliana kwamba inatengua swaumu.

Mtu akipata ugonjwa wa kutokwa na damu puani funga yake haitatenguka kwani ni jambo linalomtokea bila yeye kutaka (labda kama itamdhoofisha kwa hali ambayo hawezi kufunga na anahitaji tiba).

Kuhusu kutoka damu kwa ajili ya kung'oa jino, kufanyiwa upasuaji, kupima damu ama kupata jeraha na mengine kama hayo hayatengui swaumu isipokuwa, kama ilivyosemwa hapo juu, yatakuwa na athari kwa maana ya kumdhoofisha mfungaji.

Hata hivyo, wanazuoni wanakubaliana kwamba kupiga chuku au kutoa damu pekee hakuharibu swamu kama hakutaandamana na madhara yake (udhaifu). Katika kutoa damu kwa ajili ya kumpa magonjwa imekuwa ikishauriwa mtoaji kunywa maji mengi na vimininika, hali ambayo inaonekana kutoa damu kunaleta udhaifu wa mwili.

**KUTAPIKA**

Kujitapisha kwa makusui kunatengua swaumu. Hii inatokana na Hadithi ya Mtume (SAW) inayosema: "Yeyote anayetapika bila kukusudia hatakiwi kulipa siku hiyo isipokuwa anayejitapisha kwa makusudi."

Kujitapisha hufanyika wa kuingiza kidole hadi kooni, kubonyeza tumbo, kunusa kitu ambacho mtu anajua kinamtapisha ama kuangalia kwa makusudi kinyaa.

**HEDHI**

Jambo la saba linalotengua swaumu ni mwanamke kupata hedhi ama damu ya uzazi.

Hii ni kwa sababu Mtume (SAW) alisema: "Je, siyo kwamba mwanamke anapokuwa kwenye hedhi hapaswi kuswali wala kufunga?" al-Bukhaari, 304.

Mwanamke anapoona damu ya hedhi ama nifaas (damu ya uzazi), funga yake inabatilika hata kama ni dakika chache kabla ya muda wa kufuturu.

Lakini kama mwanamke atahisi kwamba hedhi imeshaanza lakini hajaona damu hadi kuzama kwa jua, funga yake itakuwa sahihi kwa mujibu wa wanazuoni wengi.

Kama damu ya hedhi au nifaas itakoma usiku halafu mwanamke huyo amedhamiria kufunga siku ya pili yake halafu alfajiri ikampazukia kabla hajaoga, wanazuoni walio wengi wanaona kwamba funga yake ni sahihi.

***Chanzo: IslamQA (Maswali na Majibu)***



## Kurunzi

Na Dk. Reubeni Lumbagala | 0620 800 462

# Kumbukeni kila mara cheo ni dhamana tu

"TUNAFANYA haya katika kusaidia wananchi kero zao mbalimbali ili tutakapo kufa watu wasitutafute kwenye makaburi yaliyonakshiwa na marumaru bali kwenye mioyo ya wale ambao walinufaika na sisi kutokana na haya tunayoyafanya."

Maneno hayo maarufu yaliwahi kusemwa na mfanyabiashara na kiongozi mashauri wa zamani wa Morocco, Abu Abdullah Muhammad Ibn Battutah.

Hii kwa mbali inafanana na kauli aliyoitoa wakati fulani Rais wa Awamu ya Pili Ali Hassan Mwinyi kwamba "Maisha ni historia tu. Basi jitahidi uwe historia nzuri."

Swali kwa wewe kiongozi katika ofisi ya umma, unadhani kutokana na utumishi wako, hata kabla hujaondoka duniani utakuwa historia nzuri? Utagusa mioyo ya watu watakaokuwa wanakumbuka utumishi wako uliotukuka?

Chama cha TANU (Tanganyika African National Union) kilichofanya kazi kubwa ya kuleta ukombozi Tanganyika (sasa Tanzania Bara) kiliweka ahadi zake ambazo wanachama na viongozi wake wa wakati huo na sasa CCM wanapaswa kuzielewa, kuziishi na kuzitendea. Mathalani, moja ya ahadi za za mwanachama wake ni ile isemayo "Cheo ni dhamana, sitatumia cheo changu wala cha mtu mwingine kwa faida yangu."

Kimsingi, ahadi hii ina lengo la kuwakumbusha watumishi, watendaji na viongozi kuwa nafasi walizonazo si mali yao, wala si nafasi ya kudumu, bali ni nafasi za utumishi wa umma kwa muda tu na hivyo wanawajibika kuwatumikia wananchi kutoka na kupewa dhamana hiyo na kamwe wasitumie nafasi zao au za watu wengine kwa manufaa yao binafsi.

Licha ya kuwa ahadi hii ni ya wanachama wa CCM, lakini ni ahadi ambayo inapaswa kufanyiwa kazi aliyekabidhiwa ofisi ya umma. Kwa mtumishi au kiongozi anayeelewa vyema ahadi hii na kuifanyia kazi kikamilifu, utumishi wake utaleta manufaa na faida nyingi kwa wananchi na taifa na daima atakumbukwa na kizazi cha sasa na kijacho. Kuiishi ahadi hii ni kuwatumikia wananchi kwa kuhakikisha maslahi na haki zao wanazipata kwa wakati na kamwe hatakuwa sehemu ya kukwamisha na kuzuia kabisa haki kupatikana bali kuiwezesha kupatikana.

Juzi nilimsikia Sheikh mmoja akiwaambiwa waumini wa dini ya Kiislamu ambao wanaendelea na Mfungo wa Ramadhani kuhusu Hadithi ya Mtume Muhammad (SAW) inayosema kwamba muumini anayemfurahisha sana Mwenyezi Mungu ni yule ambaye watu wengi wananufaika naye.

Kwamba kadri unavyopendwa na Mungu kutokana na waja waje wengi wanavyonufaika na wewe, ndivyo pia Mungu anavyozidi kukupa baraka za hapa duniani na kesho ahera.

Nimpongeze Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko ambaye mara kwa mara amekuwa akisisitiza uwajibikaji, uzalendo na moyo wa dhati wa kuwatumikia wananchi kwani kwa kufanya hivyo, kero za wananchi zinatatuliwa na hatimaye ufikiwaji wa mipango na malengo ya nchi unatimia kwa wakati.

Mathalani, hivi karibuni Dk. Biteko alifungua Mkutano wa Tano wa Baraza la Wafanyakazi la Wizara ya Nishati, alisisitiza kuwa cheo ni dhamana, hivyo watumishi wa Wizara ya Nishati wakiwemo Tanesco wawahudumie wananchi ili nchi iweze kusonga mbele kimaendeleo.

"Yani wewe kuwa mtu wa Tanesco au kuwa mtu wa Wizara ya Nishati unaonaje fahari kuabudiwa na kutukuzwa kwa sababu ya cheo ambacho kwanza sio chako ni cha watu… Hivi vyeo vyote mlivyonavyo kikiwemo cha kwangu sio vya kwetu ni temporary (vya muda mfupi) kwa ajili ya ku-service (kuhudumia) wakati ule. Kwa nini msijifanyie marafiki kwa vyeo mlivyo navyo? Kwa nini mnajitengenezea maadui kwa vyeo mlivyonavyo? Unafanya Tanesco ambalo ni shirika zuri la nchi linaonekana ni shirika ambalo ni baya la hovyo. Akisimama mtu wa Tanesco mahali popote watu wanaanza kucheka utafikiri kasimama comedian (mchekeshaji), kwa nini? Ni kwa sababu ya character (tabia) za watu wa mle ndani.

"Kumpelekea mtu nguzo mpaka akupe hela, na wananchi wapo wanaojua kushawishi. Atakushawishi kwa haraka zake anakwambia, bwana nisaidie niwekee nguzo hapa haraka kuna milioni hapa. Siku nguzo imesimama atakumbuka milioni yake na atakwenda kwa wengine kuwaambia wale jamaa hawapeleki nguzo mpaka milioni, unahangaika hapa, mimi nilivyomgonga milioni, mbona kesho yake ilifika. Tunaonekana wote humu wapiga dili," alisema.

Kwa viongozi wote wawe wa kuchaguliwa au kuteuliwa wana jukumu la kuwatumikia wananchi wanaowaongoza na kuhakikisha nafasi walizonazo zinakuwa ni daraja la kufanikisha maendeleo badala ya kukwamisha. Wapo wanaoelewa vyema dhana ya cheo ni dhamana na hivyo kwa wakati walionao wa kuwatumikia wananchi wanatimiza wajibu wao kikamilifu na kwa moyo wa uwajibikaji na uzalendo mkubwa.

Cheo ni kama koti la kuazima, ambalo kwa kuwa umeliazima ni lazima utalirudisha kwa wenyewe. Ni muhimu kuwa mnyenyekevu katika kuwatumikia wananchi.

Lakini pia wapo baadhi watu ambao kwao cheo ni fimbo ya kuwachapa wengine, na hivyo kutaka kuonesha umuhimu wa nafasi zao kwa kuwakwamisha wengine. Viongozi wanaotumia nafasi zao kuwaumiza wengine, wanapaswa kubadilika kwani cheo ni dhamana.

Vilevile, kwa watumishi wa umma waliopewa dhamana ya kuwatumikia wananchi wapo wanaowajibika na wapo wanaokwamisha wengine kwa nafasi walizonazo. Ninaandika makala haya ili kuwakumbusha wenye vyeo na madaraka katika ofisi za umma kuzingatia kila mara kwamba cheo walicho nacho, ofisi ya umma wanayoitumikia ni dhamana.

Wajue kwamba mshahara wanaolipwa, kiyoyozi wanachofurahia au kama kuna gari wamepewa basi vyote vinatokana na kodi za wananchi wanaovuja jasho ili wao wawatumikie. Kwamba kimsingi waajiri wao halisi ni hawa wananchi na hivyo si watu wa kusukumwasukumwa bali wanatakiwa wawatumikie.

Kwa lugha nyingine walioko kwenye ofisi za umma wajue kwamba ndio watumwa wa wananchi na si kufikiri kwamba wananchi wanapaswa kuwatumikia wao.

Biteko alipokuwa Waziri wa Madini, aliwakumbusha wakurugenzi ndani ya wizara hiyo kuacha ushamba wa kuwanyima magari watumishi wao wa ngazi za chini pindi wanapokuwa na ziara za kikazi kwa kutaka magari hayo wayatumie wao wenyewe hata kama kwa wakati huo hayana kazi ya msingi, kwani kufanya hivyo kunakwamisha maendeleo.

Nimalizie kwa kurudia kuwakumbusha wote waliopewa nafasi mbalimbali za kuwahudumia wananchi kuzingatia kuwa cheo ni dhamana tu, leo wapo kwenye nafasi hizo, kesho wataondoka wengine wataingia.

Wananchi wanataka huduma waliopewa dhamana ya kuwahudumia watimize wajibu wao kikamilifu kwa maslahi na maendeleo ya nchi yetu.

Ikumbukwe kuwa huduma bora kwa wananchi ni moja ya mkazo mkubwa unaohimizwa na Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi mahiri wa Dk. Samia Suluhu Hassan.

Asante sana Dk, Biteko kwa kuhimiza uwajibikaji na dhana ya cheo ni dhamana. Ukipewa ofisi ya umma, ukipewa cheo, ukichaguliwa kuwa mbunge, ukisoma hadi kuwa profesa usidhani kwamba wewe una uwezo, maarifa na akili nyingi kuliko Watanzania wengine, la hasha. Wapo Watanzania wanaoweza kufanya kazi hiyo ila kwa sasa Mungu amekuchagua wewe. Acha kiburi, tumikia watu ili uwe hadithi nzuri.



**Yani wewe kuwa mtu wa Tanesco au kuwa mtu wa Wizara ya Nishati unaonaje fahari kuabudiwa na kutukuzwa kwa sababu ya cheo ambacho kwanza sio chako ni cha watu...**



KLINIKI YA FIKRA

# Mambo muhimu ya kuzingatia kuhusu fedha - 1

VIJANA wanasema "fedha ndio mpango mzima" ingawa pia kuna kauli inayokinzana na hiyo ukisema fedha si msingi wa maendeleo siku zote. Misemo hii kila mmoja una muktadha wake, lakini la muhimu ni kutambua kwamba fedha inaendesha maisha yetu ya kila siku kwa kutuwezesha kufanya miamala mingi kila siku.

**1. ANZA KUYATAZAMA MAISHA YAKO BAADA YA KUSTAAFU**

Ni muhimu kuweka mipango yako ya kustaafu mapema. Jiulize maswali muhimu kama vile utahitaji kima cha chini cha shilingi ngapi kila mwezi ili uishi maisha ya kawaida mazuri ukimudu gharama yako wakati utakapostaafu?

Hii itakupa nafasi kuufungua ubongo kuanza kujiuliza njia mbalimbali ambazo unaweza kuanza kuziandaa sasa kukutengenezea fedha wakati huo. Kusahau kuutazama wakati huo wa kustaafu sasa, ni kuandaa msongo wa mawazo wakati utakapofika. Tuna masomo mazuri ya jinsi ya kujiandaa na maisha baada ya kustaafu, ukiyahitaji wasiliana nasi.

Lakini cha muhimu anza kujiuliza maswali haya ili kufungua ubongo kwa ajili ya maandalizi.

**2. TAMBUA UTOFAUTI KATI YA MAHITAJI NA MATAMANIO**

Mahitaji (Needs), ni bidhaa na huduma muhimu ambazo watu wanahitaji ili waweze kuishi. Bidhaa na huduma hizi zinajumuisha vitu kama; chakula, maji, mavazi, malazi, elimu na matibabu (kama utapatwa na ugonjwa).

Matamanio (Wants) ni bidhaa na huduma ambazo watu hutamani kuwa nazo ingawa wanaweza kuishi bila kuwa nazo na wasidhurike. Vitu hivi ni pamoja na; mapambo, urembo, starehe, na vitu (mahitaji) ya gharama kubwa, sigara, pombe, gari au simu vya bei ghali, vito vya thamani na starehe za gharama.

Ni vyema kushughulika na mahitaji muhimu na kupunguza kununua vitu visivyo vya lazima ili kuweza kuweka akiba.

**3. JALI THAMANI YA FEDHA YAKO**

Mosi, unapoamua nini cha kununua, toa kipaumbele kwa vitu muhimu ambavyo kwa dhati unavihitaji. Kisha weka akiba na kuwekeza kwa kadiri unavyoweza.

Pili, wakati wa kununua bidhaa au huduma, uwe mwangalifu kwa kuwa bidhaa na huduma zinatofautiana thamani na ubora.

Kwa bidhaa unayoihitaji hakikisha unazingatia ubora na thamani (Value for money) sambamba na gharama za uendeshaji wa bidhaa husika.

Unaweza kupata bidhaa kwa bei nzuri na ni bidhaa bora lakini gharama za uendeshaji ni kubwa kuliko uwezo wako. Ni muhimu kuwa makini na hayo mambo yote. Ili haya yote yakae vizuri, ni vyema usifanye Manunuzi kwa mihemko au kwa pupa, jipe muda, tulia na fanya utafiti wa kutosha.

Tatu, unaponunua chakula na mahitaji mengine ya nyumbani, jifunze na jitahidi kujijengea uwezo wa kununua mahitaji kwa jumla na kupunguza hali ya kununua kidogokidogo.

Manunuzi ya jumla yatakusaidia kupunguza safari za dukani, yatakusaidia kupunguza gharama lakini pia yatakujengea utaratibu na uwezo wa kufuatilia matumizi yako na kisha kujitathmini.

**4. TUNZA KUMBUKUMBU YA MATUMIZI YAKO**

Kutunza kumbukumbu ya matumizi yako inakusaidia kupanga vipaumbele vya mahitaji yako. Pia, itakusaidia kufuatilia fedha inatumika wapi zaidi (tracking records).

**5. WEKA AKIBA NA KUFANYA UWEKEZAJI KIDOGOKIDOGO**

Kwanza kabisa, akiba ni Nini?

Jibu ni kwamba akiba ni sehemu ya mapato yako iliyohifadhiwa sehemu salama kwa ajili ya matumizi ya baadaye, dharura na uwekezaji.

Je, ni upi utaratibu wa kuweka akiba?

Kuweka akiba kunafanywa kwa kupunguza matumizi yasiyo ya lazima.

Sio lazima kuweka fedha nyingi kwa wakati mmoja, unaweza kuweka sehemu ndogo ya kipato unachokipata kama akiba.

Hata ukiwa mwanafunzi, mkulima, mfanyakazi au mjasiliamali mdogo unahitaji kuweka akiba sehemu ndogo ya kipato unachopata.

Kwa kawaida fedha hiyo ikiwekwa kidogokidogo kwa mfululizo itaongezeka na kuwa kubwa na itakusaidia kwenye matumizi, dharura na uwekezaji baadaye.

Nikuibie siri, wazungu wengi tunaowaona wanakuja kutalii huku kwetu, si kwamba wana pesa nyingi isipokuwa wengi wao wni matokeo ya kuweka akiba.

Kwa mfano, mwanafunzi akiamua kujiwekea akiba ya shilingi elfu kumi kila mwezi, baada ya miezi 24 kwa maana ya miaka miwili, atakuwa na shilingi 240,000.

Kama mkulima naye ataamua kuweka shilingi elfu hamsini hamsini kila mwezi, basi baada ya miezi 24 atakuwa na shilingi 1,200,000 kibindoni.

Vivyo hivyo, endapo mfanyakazi atakuwa anaweka akiba ya shilingi lakini moja kila mwezi basi baada miezi 24 atakuwa ametunza shilingi 2,400,000.

**WAFUNDISHE WATOTO KUWEKA AKIBA**

Suala la akiba katika jamii yetu limekuwa gumu sababu jamii haikuandaliwa na kufundishwa tabia hii tofauti na wenzetu wenye ngozi nyeupe.

Ni vizuri kuwafundisha watoto kuwa na utamaduni wa kujiwekea akiba, jambo litakalowasaidia kukua wakijua umuhimu wa kuweka akiba.

Unaweza kuwafundisha kupitia vifaa vinavyotolewa na benki au taasisi za fedha kama visanduku vidogo. Aidha, kuna taasisi kama vile benki zinaelimisha watoto kuhusu kuweka akiba.

**WEKA AKIBA ILI KUONDOKANA NA MADENI**

Kuweka akiba ni moja ya njia za kuondokana na madeni. Mtu akijipanga kupitia kuweka akiba kwa matumizi yake ya msingi, hawezi kuingia kiholela kwenye madeni kwa sababu ya ada au matumizi mengine. Jiwekee utaratibu wa kuweka akiba kwa ajili ya ada za watoto.

**WEWORK CONSULT - YOUR PARTNER IN GROWTH**

*ITAENDELEA WIKI IJAYO...*





Na Hamisi Kibari

Mtanzani wa kwanza kushinda Tuzo ya Taifa ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi Bunifu

# Niko tayari kwa kifo - 23

**Chris anapolazwa hospitali ndugu zake mkewe wanafika kumjulia hali na kumweleza kitu ambacho hakuwa anakitarajia. Kwamba wamemsamehe kuhusu suala la kumuua mkewe bila kukusudia na wala hawana mpango wa kumshitaki. Joyce naye anafika wodini na kwa mshangao anasema na yeye hana mpango wa kumshitaki Chris kwa kosa la kufanya jaribio la kumuua. Lakini, licha ya kusamehewa na watu ambao wangekuwa mashahidi kusema hawana mpango wa kumshitaki, Chris anapofikishwa mahakamani anakiri kosa la kumuua mkewe bila kukusudia. Lakini siku ya hukumu ghafla anatokea mkewe ambaye Chris alijua alimuua na watu wengi wakaamini hivyo na kusababisha tafrani watu wakidhani ni msukule. Dk. Goima anaieleza mahakama kilichojiri. Anaendelea kueleza kwa nini alimdanganya Chris kuhusu kifo cha mkewe na kuanza kumchuna fedha ili kumkomoa... Endelea.**



Dk Goima alisema siku Chris alipomleta Tausi pale hospitalini akiwa hajitambui, na bahati nzuri yeye ndiye alikuwa daktari wa zamu, alimkumbuka mwanamke huyo baada ya kupoteana kwa muda mrefu na hasa baada ya Chris kumtajia jina lake.

"Mbali na kwamba nilikiwa ninamfahamu, roho iliniuma sana baada ya kugundua kwamba kapigwa namna ile na mumewe. Mimi ni mtu ninayechukia sana mnyanyaso ya kijinsia. Yaani kwa sababu wewe ni mwanaume unajiona una misuli ambayo Mungu kakujaalia unampiga mkeo, binadamu mwenziyo mithili ya kumuua. Roho iliniuma sana," akasema Dk Goima akimtupia jicho Chris kwa hasira.

Akaendelea: "Narudia, yaani kwa sababu tu wewe ni mwanaume, Mungu amekupa misuli unampiga mkeo, binadamu mwenziyo mithili ya kumuua. Roho iliniuma sana."

Daktari hyo alisema alijitahidi kumtibu Tausi na siku ya pili yake alizindukana na kisha kumsimulia jinsi mumewe alivyotekwa na hawara hadi kumleta nyumbani kwake.

"Kwa kweli roho iliniuma sana hasa baada ya kuona Tausi amekata tamaa ya maisha na amefikia kuamini kwamba wanaume wote duniani tuko kama Chris. Nilimpigia simu Chris na kumdanganya kwamba mkewe kafa ili kumtia adabu angalau kwa kumtisha kwa muda. Lakini ninashukuru alipojiingiza mwenyewe kwa kuniambia tufiche kifo chake na kwamba kama ni kuzikwa azikwe kama mtu asiyefahamika. Hapo nilizidi kuona namna huyu jamaa hapa alivyomnyama lakini niliona ipo haja ya kumrejeshea Tausi pesa ambazo wamechuma na mumewe pamoja lakini sasa anatumbua na hawara kiasi cha kumpiga na kukaribia kumuua," alisema.

Alisimulia kwamba Tausi alipotoka hospitali baada ya siku nne huku mumewe akiwa haji kumwona kujua maendeleo yake, alimpeleka kwa kificho nyumbani kwake na kumuunganisha na mkewe ambaye alikuwa katika harakati za kufungua kampuni ya kupeleka bidhaa za kulainishia mitambo (lubricants) katika nchi za Rwanda na Burundi ambako kuna uhitaji mkubwa wa bidhaa hizo.

"Takribani kila pesa aliyonipa Chris ili kuficha kifo cha mkewe nilimpa Tausi. Mara ya mwisho, alipokosa fedha nikamshauri aniuzue nyumba. Kwamba nimrudishie fedha kadhaa na kisha nyumba ibaki mikononi mwangu. Alipokubali nikajua sasa nimesharejesha nyumba kwa Tausi. Kwa hiyo nimeinunua kwa fedha zake. Ingawa tuliandikishana kwa mwanasheria na jina langu ndilo lilikuwa kwenye mauziano, lakini tayari nimeshabadilisha, nyumba sasa mmiliki ni Kenny, mtoto wao mkubwa. Hii sasa maana yake ni kwamba asingeweza kumrithisha nyumba mwanamke kwani ndipo alipokuwa akielekea. Nilifanya haya pia kusafisha jina la wanaume ambalo lilikuwa limechafuka kupita kiasi moyoni mwa Tausi.

Kwa pesa za Chris Tausi ameshirikiana na mwenziye, yaani mke wangu kuanzisha biashara. Ili kupotea machoni mwa watu hapa Tabora, Tausi amekuwa Rwanda na Burundi kwenye masoko na juzi ndio nimemwita baada ya kusikia kuna hii hukumu ili sasa ajitokeze. Alikuwa anakuja mara moja moja kuangalia nyumba ya kijana wake namna ukarabati unavyoendelea.

"Katika jambo ambalo wengi mnaweza kushangaa kidogo, mke wangu alinishauri nimuoe pia Tausi. Msiojua ni kwamba mimi na mke wangu mkubwa tulisilimu kiasi cha miaka saba iliyopita kuwa Waislamu na kisha mke wangu nilimpeleka Kenya kusoma dini. Kwa sasa ndiye shekhati wa familia.

"Alinihimiza sana kwa sababu alimwona Tausi ni mwanamke mwenye tabia na alikuwa ameamua kusilimu baada ya kufuatilia na kuujua Uislamu. Mke wangu pia anaamini kwamba sisi wanaume si rahisi kutosheka na mke mmoja... Pengine yuko sahihi.

"Kwa hiyo, Tausi baada ya leo atajivua ndoa, atapata talaka yake, atakaa eda kisha nitamwoa na yuko tayari kwa hilo... Tausi anaamini hawezi tena kuishi na mwanaume aliyekaribia kumpeleka kuzimu. Kama mheshimiwa Jaji utampa nafasi, Tausi atasema mwenyewe," alimaliza masimulizi yake Dokta Goima.

Mahakama iliendelea kutulia kimya baada ya Dk. Goima kuzungumza kila mtu akitafakari alichokisikia kiasi kwamba hata ungedondosha peni mlio wake ungesikika kila mahala katika ile mahakama ya wazi. Ilikuwa kama wanasikiliza hadithi ya kutunga yenye uongo na ukweli na si tukio la kweli.

Jaji Wesai aliinama akiandika alichokuwa akiandika huku mahakama ikiwa bado imetulia tuli. Alipoinua uso wake, Jaji huyo alimgeukia Mama Kenny: "Hebu niambie Tausi, maelezo hayo ni ya kweli?"

"Ni kweli mheshimiwa. Ni kweli kabisa," alijibu Mama Kenny na wale wenye mashaka wakazidi kuthibitisha kwamba ni yeye kwa kuwa sasa walisikia sauti yake wanayoifahamu mbashara.

"Wewe ni Tausi kweli uliyedhaniwa umekufa na si msukule?" Akauliza Jaji kwa utani.

"Ni mimi Jaji. Mimi si msukule. Nimekaa mbali na familia yangu kwa mateso makubwa lakini tulilazimika kufanya hivyo ili kumtia adabu Chris," alijibu Mama Kenny.

"Kwa nini unamwita Chris badala ya kusema mume wangu? Nimesikia hapa kwamba bado unamdai talaka. Hivyo kwa sasa bado ni mume wako, siyo?" Alizidi kuhoji Jaji.

"Mh... Kitendo cha kuniletea mwanamke chumbani kwangu, kunipiga mithili ya kuniua na kutaka nisijulikane kama nimekufa na kuzikwa kama mzoga na halmashauri ni kwamba mimi hanipendi kabisa na siwezi kulazimisha mapenzi," alisema na watu wengi mahakamani pale wakamgeukia Chris ambaye machozi yalikuwa yanamwagika. Chris akiwa bado kasimama kizimbani mithili ya mtu aliyemwagiwa maji alinyoosha mkono kutaka kusema kitu.

Jaji alimruhusu lakini alipotaka kuzungumza akajikuta analia.

Jaji aliandika maneno mawili matatu kisha akanyanyua tena uso wake. "Kwa maelezo hayo na kwa mujibu wa kesi ya kuua bila kukusudia iliyokuwa mbele yangu, ninamwachia huru mshitakiwa Chrysostom Mataruma Magati. Lakini anaweza kushitakiwa kwa kosa la kujeruhi... Hata hivyo, wewe dokta na Tausi, mnaweza kushitakiwa pia kwa kudanganya kifo cha mtu na kusababisha kesi hii ambapo gharama nyingi za serikali zimetumika... Hilo ni suala la polisi wakiona inafaa. Hata mauziano yenu ya nyumba kwa mbali ninaona kama kuna utata wa kisheria. Lakini binafsi nadhani mlifanya vyema kumtia adabu mwanamume wa hovyo kama Chris..."

Baada ya kusema maneno hayo, Jaji Wesai alinyanyuka, na watu wote walinyanyuka pale mahakamani. Mwalimu Misango akitokwa machozi ya furaha alikuwa wa kwanza kumrukia Tausi na kumkumbatia huku Jacob naye akisubiri zamu ya kumkumbatia dada yake.

*Itaendelea*

# Amadou ampongeza mpinzani kushinda urais

**DAKAR, Senegal**

MGOMBEA wa ushirika wa utawala nchini Senegal Amadou Ba, amempongeza mpinzani wake kutoka kambi ya upinzani Rais Mteule Bassirou Diomaye Faye, kwa kushinda uchaguzi wa kiti hicho, wiki moja baada ya kutoka gerezani.

Alitoa pongezi hizo baada ya kushinda katika duru ya kwanza ya uchaguzi huo uliofanyika Jumapili iliyopita nchini humo.

"Wakati tunasubiri matokeo ya uchaguzi wa rais kutangazwa rasmi, nampongeza Rais Mteule, Bassirou Diomaye Diakhar Faye kwa ushindi wake wa duru ya kwanza," alisema Ba katika taarifa hiyo.

Uchaguzi huo ulifanyika baada ya hatua ya awali ya rais anayeondoka madarakani Macky Sall kutaka kuahirisha uchaguzi na kusababisha hofu ya kuwa anataka kujaribu kushikilia madaraka.



Katika uchaguzi huo, maelfu ya Wasenegali walijitokeza katika vituo mbalimbali nchini wakisubiri kwa utulivu kupiga kura zao.

Rais wa Tume ya Uchaguzi, Abdoulaye Sylla, alisema idadi kubwa ya watu wa nchi hiyo walijitokeza kupiga kura katika uchaguzi huo.

Waangalizi kutoka mashirika tofauti walikuwepo, wakiwamo 100 wa Umoja wa Ulaya walioshiriki katika uchaguzi nchini humo.

Faye mpinzani wa viongozi walioko madarakani aliahidi kurejesha "mamlaka ya nchi" ikiwamo kupambana na ufisadi na kuleta uwiano wa kiuchumi. VOA

# Zambia yafikia makubaliano kurekebisha deni

**LUSAKA, Zambia**

ZAMBIA juzi imetangaza kuingia makubaliano ya kihistoria na wakopeshaji binafsi wanaomiliki Eurobond zenye thamani ya dola za Marekani bilioni 3.5 na kuondoa kikwazo kikubwa katika marekebisho ya muda mrefu ya deni la nchi hiyo.

"Historia imeandikwa, tunayo furaha kutangaza makubaliano na wamiliki wa Eurobond," Rais Hakainde Hichilema, alisema kupitia mtandao wa kijamii wa X na kuongeza:

"Hii ni kurekebisha deni la zaidi ya dola za Marekani bilioni 3.5 chini ya mfumo wa pamoja wa G20," alisema.

Aidha, Zambia ni mzalishaji mkubwa wa shaba barani Afrika, ilishindwa kulipa deni lake la nje la dola za Marekani bilioni 18.6 mwaka wa 2020 lakini mazungumzo hayakwenda sawa kuhusu tofauti kati ya China na wakopeshaji wa nchi za Magharibi.

Rais Hichilema alisema Desemba, mwaka jana kwamba asilimia 98 ya wakopeshaji rasmi sasa wametia saini makubaliano ya awali ya kurekebisha deni la Zambia ambalo lilikadiriwa kufikia dola bilioni 32.8 kwa 2022. VOA



Rais Hakainde Hichilema

# Hamas yashikilia msimamo

**JERUSALEM, Israel**

KUNDI la Hamas juzi wamewambia wapatanishi kwamba wataendelea kushikilia msimamo wake wa awali kuhusu kufikia makubaliano ya kusitisha mapigano ya kudumu, ikiwamo kuwaondoa wanajeshi wa Israel ndani ya Gaza na kurejea nyumbani kwa Wapalestina waliolazimishwa kuhama makazi yao.

Pia, wanaomba kile wanachoita "ubadilishaji wa ukweli wa wafungwa," wakimaanisha wafungwa wa Kipalestina kutoka magereza ya Israel kwa kubadilishana na mateka wa Israel wanaoshikiliwa Gaza.

Hata hivyo, ofisi ya Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyau, haikutoa maelezo.



Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyau

Hamas waliwasilisha mapendekezo yake kuhusu kusitisha mapigano kwa wapatanishi na Marekani katikati mwa Machi, mwaka huu, ikiwamo kujumuisha, kuachiwa kwa mateka wa Israel kwa kubadilishana na kuachiwa huru kwa wafungwa wa Palestina 100 kati yao ambao wanatumikia vifungo vya maisha gerezani.

Baraza la Usalama la Umoja Mataifa Jumatatu iliyopita lilipitisha azimio linaloomba kusitishwa mapigano mara moja kati ya Israel na Hamas baada Marekani kujizuia kupiga kura, hali ambayo inaleta mtafaruku na mshirika wake Israel. VOA

# Ukata watishia vikosi SADC kuondoka Msumbiji

**MAPUTO, Msumbiji**

WANAJESHI kutoka Muungano wa Kanda ya Kusini mwa Afrika wanaowakilisha nchi zao kukabiliana na waasi wa Kiislamu nchini Msumbiji wanatarajiwa kuondoka nchini humo kutokana na changamoto ya kifedha.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Msumbiji Veronica Macamo, alisema Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (Sadc) ina utaratibu wa kuzingatia ukomo wa bajeti yake.

Alisema umoja huo unaamini kuwa Msumbiji iko shwari tofauti na mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), kwa kuwa inakabiliwa na makundi yenye silaha kwa miongo kadhaa sasa.

Vikosi vya kijeshi vya Sadc vinapambana kuzima ghasia nchini Congo tangu Desemba, mwaka jana.

Rais wa Msumbiji, Filipe Nyusi alisema Sadc inapanga kuondoa vikosi vyake nchini mwake Julai, mwaka huu.

Hata hivyo, Rais alisema, hatua hiyo haina maana kwamba vita vya taifa dhidi ya makundi ya kijihadi vitamalizika.

"Nchi hizo pia zimejitolea kufanya kazi nasi kwa pande mbili, ikiwa ni sawa," aliandika kwenye ukurasa wake wa mtandao wa Facebook.

"Kama Wanasumbiji tunahitaji kuwa tayari kwa ukweli huu. Tusikengeuke, jukumu kubwa liko kwetu," alisema.

Kundi la waasi lililojihami lilishambulia eneo la kaskazini mwa Msumbiji kwa miaka sita, huku kundi la Islamic State likisema ndilo lililohusika na baadhi ya ghasia hizo.

Uasi huo, ambao unahusisha mashambulizi kadhaa dhidi ya umma na vikosi vya jeshi, ulisababisha majibu ya kijeshi Julai, 2021.

Awali Rwanda ilikuwa nchi ya kwanza kupeleka kikosi chake kikiwa na zaidi wanajeshi 2,000 nchini Msumbiji na baadaye vikosi kutoka Sadc.BBC



Rais wa Msumbiji, Filipe Nyusi

# Historia ya soka la Afrika imebebwa na mashujaa hawa









**Na Valensi Mbaga**

AFRIKA ina historia kubwa katika ulimwengu wa soka. Mataifa mbalimbali ndani ya Bara la Afrika, yametoa matukio mengi ya ajabu na vipaji vikubwa katika ulimwengu wa soka.

Wengi watakumbuka jinsi Senegal ilivyotinga hatua ya robo fainali mwaka 2002 huko Korea Kusini na Japan, ambayo ilijumuisha ushindi maridhawa dhidi ya Ufaransa.

Nani angeweza kumsahau Asamoah Gyan? Mshabuliaji huyo wa zamani alijulikana zaidi kwa kuwa bora kwa nchi yake kuliko vilabu vyake vya zamani. Kwa hiyo, ikizingatiwa ni nyakati ngapi za kukumbukwa ambazo mataifa haya yamefanya vizuri kwa miaka mingi, itapita bila kusema kwamba Bara la Afrika limetoa wachezaji wenye vipaji.

Kuanzia kwa George Weah hadi Jay-Jay Okocha, na hata Nwankwo Kanu, lakini pia wachezaji wengi kutoka Afrika, wameendelea kuimarika katika ngazi ya vilabu kote duniani, huku wengi wakipata sifa nyingi katika maisha yao ya soka. Wafuatao ni wachezaji 10 bora wa Afrika wanaokumbukwa kila wakati katika historia ya soka.

**10: ROGER MILA**

Roger Milla anafahamika zaidi kwa kusherehekea kwenye kibendera cha konakwa staili ya aina yake. Hata hivyo, ni sawa kusema kwamba aliweka soka la Afrika kwenye ramani wakati wa siku zake kama mtaalamu.

Mshambuliaji huyo wa zamani, alikuwa hodari nchini Ufaransa kwa vilabu vya Monaco, Bastia na Montpellier. Katika miaka ya 1980, alikuwa kiongozi na mchezaji muhimu waliposhinda AFCON mbili mwaka 1984 na 1988, akimaliza kama mfungaji bora.

Wengi wanaweza kuwa tayari wanalijua hili, lakini anasalia kuwa mchezaji mzee zaidi kuwahi kufunga kwenye Kombe la Dunia. Licha ya kuwa na umri wa miaka 42 wakati huo, bado alikuwa akifunga mabao katika kiwango cha juu, akifunga dhidi ya Urusi kwenye mashindano ya 1994 nchini Marekani.

Hadi leo, Milla anachukuliwa kuwa mmoja wa wachezaji bora wa Kiafrika wa wakati wote.

**9: NWANKWO KANU**

Kanu hakuwa mfungaji mahiri kwa vyovyote vile, lakini ilikuwa vigumu kufahamu jinsi Kanu, akiwa na urefu wa futi 6 na inchi 6, aliweza kusonga kwa umaridadi na kufanya makubwa katika historia ya soka.

Alipata sifa nyingi kwa mtindo wake usio wa kawaida ambao ulimfanya apate mafanikio makubwa akiwa na Ajax, akishinda mataji mengi ya Uholanzi na Ligi ya Mabingwa, ambayo ilifuatiwa na kipindi kibaya ndani ya Inter Milan kabla ya kujiunga na Arsenal mwaka 1998.

Mshambulizi huyo wa Nigeria, aliongeza katika mkusanyiko wake wa taji na mataji mawili ya ligi akiwa na Arsenal kabla ya kunyanyua Kombe la FA akiwa na Portsmouth mwaka wa 2008.

Mara nyingi akionekana akicheza na tabasamu kubwa usoni mwake, Kanu ni mmoja wa magwiji wakubwa wa Ligi kuu ya England na mtu mashuhuri kumtazama akiwa uwanjani.

**8: JAY-JAY OKOCHA**

Okocha bila shaka ni mmoja wa wachezaji walotoa burudani na wakali zaidi enzi zake akicheza Ligi Kuu.

Mashabiki wa Bolton Wanderers wangetoa chochote ili kurejea mwanzoni mwa miaka ya 2000 walipokuwa wakisimamiwa na Sam Allardyce na walikuwa na wachezaji bora kama Okocha, Youri Djorkaeff na Fernando Hierro katika safu zao.

Kuna wachezaji wachache mno linapokuja suala la uchezaji.

Mashabiki wa Bolton hawakuchoka kumtazama Okocha akiingia uwanjani. Ilikuja mshangao kwamba nyota huyo wa Nigeria alihamia timu ya Uingereza kwa uhamisho wa bure kutoka Paris Saint-Germain, lakini hakika hakukatishwa tamaa wakati akiwa na klabu hiyo. Ingawa hakuwa na mataji mengi kwa jina lake, Okocha bado alitawazwa Mwanasoka Bora wa Afrika wa Mwaka mara mbili.

**7: SADIO MANE**

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Senegal, alianza safari yake katika ligi ya daraja la kwanza England akiwa na Southampton, ambapo alifunga hat-trick ya kasi zaidi kuwahi kutokea katika Premier League kwa dakika mbili na sekunde 56 Mei 2015 rekodi ambayo bado ipo hadi leo.

Bila shaka ni mmoja wa wachezaji bora wa Ligi Kuu mwishoni mwa miaka ya 2010 na mwanzoni mwa 2020.

Ingawa mafanikio yake ya mapema yalikuja akiwa na Liverpool ambapo alisaidia sana Reds kushinda taji lao la kwanza la ligi katika miongo mitatu.

Fowadi huyo, ambaye kwa sasa

>>>Inaendelea Uk. 21



# Historia ya soka la Afrika imebebwa na mashujaa hawa




>>>Inatoka Uk. 20






anacheza pamoja na Cristiano Ronaldo katika klabu ya Al-Nassr kufuatia msimu mmoja akiwa na Bayern Munich, ni mchezaji wa pili wa8 Afrika mwenye mabao mengi zaidi katika historia ya Ligi Kuu akiwa amefunga mabao 111.

**6: ABEDI PELE**

Abedi Pele anajulikana kwa kasi yake, udhibiti wa karibu, na chenga chenga, alikuwa kiungo mshambulizi mwenye neema na akili.

Licha ya kutoonekana kwenye Kombe la Dunia akiitumikia timu yake Ghana, bado alifurahia mafanikio mengi katika ngazi ya klabu.

Mwanasoka huyo bora wa Afrika mara tatu alijijengea urithi mkubwa nchini Ufaransa akiwa na Marseille.

Wakati akiwa na miamba hao wa Ufaransa, alishinda mataji matatu ya ligi na Ligi ya Mabingwa, akiwashinda wababe wa Serie A, AC Milan.

Licha ya kuwa hajawahi kushiriki Kombe la Dunia, aliweza kucheza katika Kombe la Mataifa ya Afrika mnamo 1982. Muongo mmoja baadaye, katika mashindano hayo hayo, alishinda Mpira wa Dhahabu huku Black Stars ikianguka kwenye fainali dhidi ya Ivory Coast.

**5: YAYA TOURE**

Wakati akijitengenezea jina nchini Uhispania akiwa na wababe wa La Liga Barcelona, siku nyingi za mafanikio za Toure zilikuja wakati akiwa na Manchester City, na akawa mwanzilishi wa kawaida wa timu, akicheza jukumu muhimu katika kusaidia klabu kushinda mechi yao ya kwanza kuwahi kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu mwaka wa 2012.

Kilele cha uwezo wake kilikuja msimu wa 2013/14 alipofunga mabao 20 ya ligi na kuiongoza City kutwaa taji lao la pili la Ligi Kuu.

Ni mfano bora wa mchezaji aliyeibuka upya kutoka kuwa mchezaji wa ulinzi asiyethaminiwa katika klabu ya Barcelona hadi kuwa kiungo bora wa kati (Box to box) nchini Uingereza.

Muda wake wa miaka minane nchini Uingereza ulimwona Toure kuwa mmoja wa wachezaji bora zaidi wa Manchester City wakati wote. Pamoja na hayo, bila shaka atashuka kama mmoja wa wachezaji bora wa kigeni kucheza England.

**4: DIDIER DROGBA**

Bila shaka, mmoja wa wachezaji bora wa Kiafrika kuwahi kutokea ni Didier Drogba ambaye alichangia sana kuinuka kwa Chelsea chini ya Jose Mourinho.

Mchezaji huyo mkubwa wa Ivory Coast alifunga mabao 104 kwenye ligi, mara nyingi katika hali ya hatari. Lakini alikuwa mshambuliaji hodari ambaye aliwanyanyasa mabeki kwa nguvu zake kubwa na uwezo wake wa angani.

Licha ya kushinda Kiatu cha Dhahabu katika Kombe la Mataifa ya Afrika mwaka wa 2012, akiwa na Ivory Coast ilishindwa kushinda michuano hiyo.

Wakati wake mkubwa akiwa amevalia jezi ya Chelsea, ulikuwa katika fainali ya Ligi ya Mabingwa wakati bao lake la dakika za mwisho la kusawazisha dhidi ya Bayern Munich hatimaye kuwafanya The Blues kunyakua ushindi wao wa kwanza kabisa katika shindano hilo.

**3: SAMUEL ETO'O**

Anajulikana kwa kuwa fowadi mwenye kasi, hodari, na mwenye nguvu ambaye alikuwa sahihi kwa miguu yote miwili pamoja na kichwa chake.

Mfungaji hodari na hodari wa mabao, Eto'o bila shaka alikuwa mmoja wa washambuliaji bora zaidi duniani wakati alipokuwa Barcelona na Inter Milan.

Mafanikio yake makubwa yalikuja msimu wa 2009/10 ambapo alicheza jukumu kubwa kwa Inter ya Mourinho waliposhinda mataji matatu ya kihistoria, pamoja na Ligi ya Mabingwa. Mwaka huo, alichezeshwa zaidi kama winga au hata kama kiungo mkabaji ambayo inaonyesha jinsi alivyokuwa mahiri katika ubora wake.

Kwa Cameroon, mafanikio yake ya kujivunia kwa taifa lake yalikuja mwaka wa 2000, waliposhinda medali ya dhahabu kwenye Michezo ya Olimpiki ya 2000, na kuishinda Uhispania kwenye fainali.

Katika mwaka huo huo, pia alishiriki katika mafanikio ya nchi hiyo kwenye Kombe la Mataifa ya Afrika. Ushindi wa pili wa Eto'o katika mchuano huo ulikuja miaka miwili tu baadaye.

Yote kwa yote, ni sawa kusema fowadi huyo wa zamani alikuwa na taaluma ya kipekee na anachukuliwa kuwa mmoja wa wachezaji bora wa Kiafrika wa wakati wote.

**2: GEORGE WEAH**

Wakati wa miaka ya 1990, George Weah alichukuliwa kuwa mmoja wa washambuliaji bora zaidi ulimwenguni. Alisifiwa kwa kasi yake, kiwango cha kazi pamoja na sifa zake za kimwili.

Weah alikuwa na jicho la kufunga na kwa hakika alijitahidi sana kuziba pengo la mshambuliaji wa Milan Marco van Basten.

Akipokea tuzo nyingi za kibinafsi wakati wa enzi zake za uchezaji, mwanasoka huyo wa zamani wa Afrika mara mbili alishinda Ballon d'Or mwaka wa 1995.

Ingawa washambuliaji wengi wakati huo walikuwa na mwelekeo mmoja, Weah alitofautiana nao kwani alipenda kufanya kazi nje ya boksi na kukimbia kuelekea ndani ya penalti boksi ikionyesha kuwa kero kwa mabeki pinzani.

**1: MOHAMED SALAH**


Ingawa alisahaulika huko Stamford Bridge, amefanikiwa kuwa mmoja wa wachezaji bora zaidi ulimwenguni akiwa na Liverpool.

Akiwa na zaidi ya mabao 100 katika kampeni zake tano za mwisho za Ligi Kuu ya Uingereza akiwa na The Reds, kiwango cha Mohamed Salah kimeifanya timu ya Klopp kufikia kiwango kingine katika miaka ya hivi karibuni, huku akifikisha mabao baada ya kufunga na kumaliza kipindi cha miaka 30 cha kungoja ubingwa mwaka 2020.


Kuwa winga na bado kuvunja rekodi kadhaa za ufungaji ni jambo la ajabu sana. Bila shaka, mmoja wa washambuliaji kamili zaidi kwenye mchezo. Akiwa na sifa nyingi kwa jina lake, Salah bado ana mengi ya kutoa, na ni wazo la kutisha kuona ni nini ataendelea kufikia kabla ya kuamua kuiita taaluma.

Pamoja na wachezaji hao wapo magwiji mbali mbali ambao wamefanya makubwa katika historia ya soka la Afrika ikiwemo Michael Essien, Riyad Mahrez, Pierre-Emerick Aubameyang, Kolo Toure na Emmanuel Adebayor.

# Bongo Fleva yaanza kurudi kwenye reli







**Na Valensi Mbaga**

BAADA ya kipindi kirefu cha utawala wa muziki kutoka nchini Afrika Kusini (amapiano) kutawala soko la muziki kwa kiwango cha juu, taratibu kabisa tumeanza kuona wasanii wa Tanzania wakikumbuka na kurudi walipotoka kwenye ladha ya bongo fleva halisi.

Tasnia ya muziki wa Bongo Fleva imeona ongezeko la wasanii wengi kurejea katika muziki wa asili ya Tanzania na kuondoka katika utumwa wa ladha ya muziki wa kigeni.

Hii imeleta ladha mpya na tofauti katika muziki wa Tanzania, huku wasanii wakileta ubunifu na upekee katika kazi zao mpya.

Hali hiyo pia ilimuibua, Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Hamis Mohamed Mwinjuma maarufu MwanaFA na kuandika "Inafurahisha kwamba hits kubwa zaidi mbili za muziki wa bongo muda huu #Dah na #Mapoz siyo amapiano. Pengine tumestukia tumeamua kurudi kwenye reli. Big up".

Wasanii mbalimbali ikiwemo mwanamuziki mashuhuri anayetawala soko la muziki wa Tanzania kwa sasa, Diamond Platnumz (Simba la Masimba Dangote), ni mmoja kati ya wasanii wanaoongoza kubadilisha upepo huo.

Ubunifu mpya katika nyimbo mpya zinazozalishwa kwa sasa, ndizo zinarudisha ladha halisi ya bongo fleva iliyopotea kwa kipindi kirefu.

Nyimbo kama "mapoz" kutoka kwa Diamond Platnumz akimshirikisha Mr. Blue na Jay Melody ambayo imepata kuangaliwa na watu milioni 5.9 tangu Februari, mwaka huu.

Ngoma nyingine zilizopata ufuatiliaji mkubwa ni pamoja na 'Dah!' ya mwanadada Nandy akimshirikisha Ali Kiba iliyopata wafuasi milioni 6.6, 'Down' kutoka kwa Rayvanny,1.48M, 'Umechelewa' ya Mbosso 728K.

Nyimbo nyingine ni 'Dharau' kutoka kwa Ibraah akimshirikisha Harmonize iliyopata wafuasi milioni 1.06, 'Number One' ya Billnass ft Mbosso ikiwa na 204K, 'Away' kutoka kwa Marioo (Bad) akimshirikisha Harmonize yenye watazamaji milioni 1.06.

Pamoja na 'Zawadi' ya bibie Zuchu akimshirikisha Dadiposlim yenye watazamaji 437K,'I Made It' ya Harmonize akimshirikisha Bobby Shmurda na Bien ambayo imekusanya watazamaji million 2.5 na 'Nisiulizwe' ya Afrikan Boy Jux yenye watazamaji 983K pamoja na nyingine nyingi.

Kwa pamoja kazi hizi kutoka kwa wasanii hawa na wengine wengi zimeleta chachu kubwa ya kurudisha ladha halisi ya muziki wa Tanzania (Bongo Fleva).

# Mkwasa: Makocha wazawa, wakiwezeshwa wanaweza

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya timu ya taifa 'Taifa Stars' kuichapa Mongolia bao 3-0 kwenye mechi ya FIFA Series 2024, kocha wa zamani wa timu hiyo, Charles Boniface Mkwasa, amewapongeza makocha wazawa Hemed Suleimani 'Morocco' na msaidizi wake, Juma Mgunda kwa kuongoza mauaji hayo.

Akizunguza jijini Dar es Salaam jana, Mkwasa alitanabahisha kwamba makocha wazalendo, ndiyo wanaoweza kuiletea Stars mafanikio ya juu, lakini tatizo ni mizengwe iliyokithiri kwenye soka la Tanzania linalosababisha makocha hao wasiaminiwe.

Nyota huyo wa zamani wa Yanga na Taifa Stars ambaye pia amewahi kuwa kocha na kiongozi wa Wanajangwani, alisema wapo makocha wengi wazalendo wenye sifa na uwezo wa kufundisha timu za taifa kuanzia za vijana hadi ile ya Taifa Stars wakipewa hiyo fursa kikamilifu.

Akifafanua juu ya imani yake kwa makocha wazawa, Mkwasa alieleza kuwa, mbali ya makocha hao kufahamu mazingira halisi ya nchi na wachezaji, lakini pia urahisi wa mawasiliano baina ya wachezaji na makocha hao wazalendo huwa ni wa uhakika.

"Mara nyingi makocha wa kigeni wanaokuja hapa Tanzania, huongea zaidi lugha za Kiingereza au Kifaransa, jambo ambalo limekuwa tatizo kubwa kwa wachezaji, inabidi watumike wakalimani ambao hata hivyo, wengine hushindwa kuwasilisha kwa ufasaha kile wanachotaka walimu hao," alifafanua Mkwasa.

Mkwasa ambaye ni kocha wa mwisho mzawa kuwa Kocha Mkuu wa Stars amelitaja tatizo lingine wanalokabiliana nalo makocha wazalendo wanapopewa timu za taifa au kufundisha klabu kubwa za Tanzania kwamba, huwa hawapewi mahitaji muhimu na mazingira mazuri ya kufanya kazi kama inavyokuwa kwa makocha wa kigeni.

"Viongozi huwa wanawakwamisha makocha wazawa, aidha kwa kutokujua au kwa kudhamiria, sisi huwa hatulipwi vizuri na wakati mwingie hatulipwi kabisa, mfano ni mimi mwenyewe hadi leo bado nadai maslahi yangu pale TFF, lakini haitokei hivyo kwa makocha wazawa," alifichua Mkwasa.


Mkwasa ambaye enzi zake akicheza soka alikuwa maarufu kwa jina la 'Master' kutokana na kucheza soka maridhawa katika nafasi zaidi ya moja uwanjani, pia aliweka wazi kuwa makocha wazawa huwa wanaangushwa kwa kutopewa vitendea kazi vya kutosha kama inavyokuwa kwa wageni ikiwemo mipira michache na vifaa vingine muhimu vya mazoezi.

Stars juzi ikiwa chini ya Hemed 'Morroco' na Juma Mgunda baada ya Shrikisho la Soka Afrika (CAF) kumfungia Kocha Mkuu Mtunisia Adel Amrouche mechi nane kufuatia kutoa kauli tata wakati wa michuano ya Mataifa ya Afrika (AFCON) kule Ivory Coast, iliifunga timu ya taifa ya Mongolia bao 3-0.

Katika mechi ya awali ya mechi za FIFA Series 2024 zinazochezwa Katika Jiji la Baku nchini Azerbaijan, Stars ilifungwa na Bulgaria bao 1-0.



Charles Boniface Mkwasa



## Kona ya Urembo

Na Hidaya Machuppa Simu: +255 765 828 219

# Kuvaa kwa Mamlaka



UKWELI mmoja unabaki thabiti katika uongozi: mwonekano wako unazungumza mengi kabla hata ya kusema neno. Viongozi wa kike wanaotaka kuwa viongozi wanaelewa umuhimu wa kuonyesha mamlaka, taaluma na kujiamini katika kila nyanja ya maisha yao. Na moja ya zana zenye nguvu zaidi wanazo nazo ni nguo zao za nguo. Makala haya yataangazia sanaa ya kuvaa kwa mamlaka, kutoa mikakati ya vitendo na vidokezo vya kukusaidia kung'aa katika safari yako ya uongozi.

Uongozi ni zaidi ya maneno na vitendo; inahusisha kila sehemu ya uwepo wako, kutia ndani jinsi unavyoonekana na jinsi unavyovaa. Ingawa ni muhimu kuongoza kwa umahiri, uadilifu, na maono, mwonekano wako pia una jukumu muhimu katika kuwasilisha mamlaka, imani na taaluma. Katika makala haya, tutachunguza kwa nini kuangalia na kuvaa kama kiongozi ni muhimu na kutoa orodha ya vitu vitano vinavyopendekezwa kwa WARDROBE ya kiongozi.

### Kuelewa nguvu ya WARDROBE

Kabla ya kuzama katika maelezo mahususi, ni muhimu kufahamu ushawishi mkubwa ambao mavazi hushikilia. Mavazi yako yanaweza kuunda mitazamo, kuongeza kujiamini, na kukusaidia kudhihirisha mamlaka bila shida. Unapovaa kwa kusudi na nia, unatuma ujumbe wenye nguvu kwamba uko tayari kuongoza.

### Kanuni za msingi za kuvaa kwa Mamlaka

Kujiamini ni sifa muhimu kwa kiongozi yeyote. Mavazi yako yanapaswa kuakisi na kuboresha hali yako ya kujiamini. Chagua vipande ambavyo vinakufanya ujisikie nguvu na raha. Suti zilizotengenezewa, nguo zilizotoshea vizuri, na vifuasi vya ujasiri vinaweza kuongeza ujasiri wako.

Pamoja na kujiamini, taaluma pia ni jambo lisiloweza kujadiliwa katika uongozi. Wekeza katika ubora wa juu, vipande vya kawaida vinavyoonyesha umahiri na kutegemewa. Blazi nyororo, blauzi zisizo na wakati, na viatu vilivyosafishwa ni bidhaa kuu za WARDROBE za kitaalamu. Kumbuka, umakini kwa undani ni alama ya kiongozi wa kweli.

### Sanaa ya kujenga WARDROBE inayotumika mengi

Wakati wa kujenga WARDROBE yako, zingatia vipande visivyo na wakati ambavyo vinastahimili mitindo inayobadilika kila wakati. Blazi iliyoundwa vizuri, nguo nyeusi ndogo, kama vile vazi la Lemaire midi, na mkoba bora ni uwekezaji ambao hulipa kwa muda mrefu. Vitu hivi vinaweza kuchanganywa na kuunganishwa ili kuunda aina mbalimbali za mavazi ya maridadi.

WARDROBE ya aina nyingi hauhitaji mkusanyiko mkubwa wa nguo. Kukubali dhana ya WARDROBE ya capsule, ambapo vipande vichache muhimu vinaweza kuunganishwa kwa njia nyingi. Hii hurahisisha chaguzi zako za kila siku na kuhakikisha unaonekana kuwa pamoja kila wakati.

### Mavazi kwa ajili ya tukio

Katika mipangilio ya kampuni ya hali ya juu, kuvaa kitaalamu hakuwezi kujadiliwa. Chagua suti zilizowekwa maalum za rangi zisizo na rangi, mashati meupe na visigino vilivyofungwa. Zingatia ufaao na ubora wa mavazi yako, kwani maelezo haya yanawasilisha umahiri na umakini kwa undani.

Unaweza kuonyesha mtindo wako kwa matukio ya mitandao, makongamano, na mikutano ya nje ya tovuti huku ukidumisha mamlaka. Zingatia vipande vya kauli, kama vile skafu ya ujasiri au vito vya kifahari, ili kuongeza mguso wa utu kwenye mavazi yako ya kitaalamu - mtindo wa kusawazisha kwa ujasiri unaotokana na kuvaa kwa kusudi.

### Vidokezo vitendo vya utunzaji wa WARDROBE

Kudumisha wodi ya kitaalamu ni muhimu kama kujenga moja. Kagua nguo zako mara kwa mara kama zimechakaa na kuchakaa, na uwekeze kwenye utunzaji unaofaa, kama vile usafishaji wa nguo na utunzaji wa viatu. Panga WARDROBE yako kwa ufikiaji rahisi wa vipande muhimu, uhakikishe kuwa uko tayari kila wakati kukabiliana na changamoto yoyote ya uongozi inayokuja.

Katika safari ya uongozi, WARDROBE yako inapaswa kuonekana kama mshirika, sio mawazo ya baadaye. Kwa kuvaa kwa mamlaka, unaboresha picha yako ya kitaaluma na kuongeza uwepo wako wa kujiamini. Kama kiongozi wa kike anayetaka kuwa kiongozi, tumia mikakati hii ya kabati kwa manufaa yako, ukionyesha kujiamini, taaluma na mamlaka katika kila hatua. Chukua hatua leo, na acha mavazi yako yaakisi kiongozi unayetamani kuwa.

Kumbuka, kuvaa kwa mamlaka sio kufuata; inahusu kutumia nguvu ya mavazi ili kukuza sifa na nguvu zako za kipekee kama kiongozi wa kike.

> **UONGOZI** ni zaidi ya maneno na vitendo; inahusisha kila sehemu ya uwepo wako, kutia ndani jinsi unavyoonekana na jinsi unavyovaa. Ingawa ni muhimu kuongoza kwa umahiri, uadilifu, na maono na mwonekano.


Leo yetu ndiyo kesho yetu

# Uelekeo Spoti

| Jumatano Machi 27 - Aprili 02, 2024 |

# Vinicius Jr aumizwa na Ubaguzi wa rangi

**MADRID,Hispania**



MCHEZAJI Vinicius Junior anaekipiga katika klabu ya Real Madrid amedondosha chozi alipokuwa akijibu kuhusu masuala ya ubaguzi yanayoendelea Hispania dhidi yake

"Sijawahi kufikiria kuondoka Hispania kwa sababu ya maneno ya watu wabaguzi, itawapa nguvu na kupata wanachokitaka, Sitaondoka hapa kwenye klabu bora zaidi Duniani, Nitabakia Imara kwa sababu Rais na Klabu wananiunga mkono"


"Nimekuja hapa kucheza mpira tu na nitafanya hivo kwa ajili ya familia yangu mashabiki na klabu yangu na sio vinginevyo sitakata tamaa" Alisema wakati akijibu swali hilo

Mara kadhaa Vini amekuwa akikumbana na vitendo vya ubaguzi wa rangi katika mchezo wa soka.

# P Didy akutwa na majanga

**LOS ANGELES, Marekani**

MWANAMUZIKI na Mfanyabiashara maarufu Sean "Diddy" Combs ameanza kutafutwa na polisi ambapo baada ya polisi kuvamia makazi yake ya Los Angeles na yale ya mjini Miami wakimtafuta mkongwe huyo, aonekana akitangatanga.



Maafisa wa Idara ya Mambo ya Ndani wamechukua hatua za kisheria katika miji ya New York, Los Angeles, na Miami kufuatia uchunguzi wa mashtaka ya unyanyasaji wa kingono yanayomkabili tangu mwaka jana.

Katika tukio hilo, watoto wake wawili wa kiume, Justin na King Combs, wametiwa nguvuni na askari, wakionekana wamefungwa pingu.

Kumekuwa na kesi kadhaa dhidi ya Diddy kuhusu unyanyasaji wa kijinsia, lakini wanasheria wake wamekanusha tuhuma hizo.



# Ulimwengu na Nyoni wafutiwa kadi nyekundu

**Na Mwandishi Wetu**

MSHAMBULIAJI wa Singida Fountain Gate FC, Thomas Ulimwengu amefutiwa adhabu yake ya kadi nyekundu aliyoipata kwenye mchezo dhidi ya Namungo FC.

Kadi hizo zimefutwa baada ya bodi kujiridhisha kuwa hazikupaswa kuwa kadi nyekundu.

Pia kiungo Erasto Nyoni wa Namungo FC naye amefutiwa adhabu yake ya kadi nyekundu aliyoipata katika mchezo dhidi ya Singida FG.

Bodi ya ligi kupitia kwa Mtendaji wake Mkuu, Almasi Kasongo wamedhihirisha kuwa imeshawatumia barua rasmi Singida Fountain Gate FC.

# Simba yakutwa na balaa zito




**Na Mwandishi Wetu**



KLABU ya Simba imetozwa faini ya Sh. milioni moja kwa kosa la mashabiki wake pamoja na walinzi wake wa uwanjani (stewards) kupanga njama na kufanikisha azma ya kuingia uwanjani na kufanya vitendo vinavyoashiria imani za kishirikina wakati wa mchezo dhidi ya Mashujaa katika dimba la Azam Complex Machi 15, mwaka huu.

Taarifa ya Idara ya Mawasiliano ya Bodi ya Ligi kuu (TPLB) imebainisha kuwa mashabiki hao walionekana kupitia video fupi iliyosambaa mitandaoni, wakijadiliana na mlinzi wa uwanjani (steward) kabla hawajaingia uwanjani kufanya tukio hilo lililoleta taswira mbaya.

Aidha, walinzi wa uwanjani wa klabu ya Simba, Kessy Mohamed, Mrisho Mindu Pamoja na Mohamed Salmin pamoja na shabiki aliyefahamika kwa jina la Mohamed Saleh, wamefungiwa kuingia viwanjani kwa kipindi cha miezi 12 kwa kosa la kushiriki katika tukio la mashabiki kuingia uwanjani wakati mchezo wa mchezo huo uliomalizika kwa Simba Sc kushinda 2-0.

"Bodi inaendelea na uchunguzi wenye lengo la kufahamu wahusika wengine wa tukio hilo ambao hawakutambulika mara moja ili wachukuliwe hatua kali za kikanuni." ilisema taarifa hiyo.

Klabu ya Simba inawajibika kuhakikisha mashabiki na viongozi walioadhibiwa wanatii adhabu zao na kuzitekeleza kikamilifu ili kuepuka klabu kuadhibiwa zaidi.

"Bodi ya Ligi Kuu Tanzania, inalaani vikali vitendo vinavyoashiria imani za kishirikina vinavyofanywa na wachezaji, mashabiki na maafisa wa klabu kwani vitendo hivyo vimekuwa vikichafua taswira nzuri ya Ligi pamoja na kushusha hadhi ya Ligi yenyewe.